CHUO CHA BIBLIA

VITABU VYA
1 & 2 WAKORINTHO

KITABU CHA 13

SURA YA KWANZA

Muhtasari Wa Waraka Wa Kwanza Wa Paulo Kwa Wakorintho

Waraka wa Kwanza Paulo aliouandika kwa Wakorintho unafanana na nyaraka zake, za uchungaji alizoandika kwa Makanisa ambayo aliyaanzisha wakati wa huduma yake kama mmishionari mkuu na mpanzi wa Makanisa aliyewahi kuwepo katika historia ya Kanisa la Yesu Kristo. Waraka wake kwa Warumi ulikuwa bora sana wa kithiolojia na unagusia mambo yote yaliyo sahihi kwa kundi la waumini ambao hakuwa amekutana na hapo awali. Hata hivyo, nyingi za nyaraka zake zilikuwa zimeandikwa kwa mtazamo wa uchungaji kwa Makanisa aliyofahamu vyema, hata kurekebisha shida au kufunza pamoja na kuwatia moyo waumini katika imani yao. Waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorintho unalingana na nyaraka alizoandika kwa Makanisa ambayo alifahamu vyema, hata kurekebisha makosa yao.

Sehemu Ya Urekebishaji Ya Waraka
(Sura Ya Kwanza Hadi Kumi Na Moja)

Paulo ndiye mwanzilishi wa Kanisa la Korintho katika safari yake ya pili ya umishionari (**Matendo 18**). Kwa muda mfupi katika makazi yake huko Efeso, Paulo aliweza kutembelea Kanisa hilo la Korintho kwa mara ya pili. Ilikuwa ni katika mara hii ya pili ambapo baadhi ya washirika wa Kanisa hilo walipomfahamisha baadhi ya shida na matatizo yaliyowakumba katika Kanisa baada yake kuondoka huko. Waraka wa Paulo wa kwanza kwa Wakorintho hugusia matatizo yale na kuwaonyesha jinsi ya kuyarekebisha.

Kando na shida zao nyingi, Paulo alitambua kwamba waumini wa Korintho walikuwa *'wametakaswa katika Kristo Yesu'* na *'kuitwa kuwa watakatifu* (**1:2**).' kutokana na jinsi Paulo alivyowataja katika waraka huu, tunaweza kujifunza kitu fulani kuhusu maana ya neno 'kutakaswa.' Maana sahihi ya neno hili ni, 'kutengwa kando.' Watu waliotakaswa sio watu wakamilifu ila ni watu ambao wametengwa kumfuata Kristo. Kwa

kuwa Wakorintho walikuwa wameitwa ili kumwakilisha Kristo humu duniani kama aliyewaongoza washiriki wake waliosajiliwa kwa Kanisa hili la imani, Paulo aliuchukuwa huu kuwa wajibu wake kuwafunza hawa Wakorintho jinsi wanavyostahili kuishi.

Sura za kwanza kumi na moja katika Wakorintho wa kwanza zinazungumzia shida zinazotambulikana ambazo Paulo alifahamu kuwa zilikuwa zimekumba Kanisa na kuzuia kukua pamoja na ushuhuda wao; kibinafsi, na kama Kanisa katika mji wa Korintho. Kwa kukagua shida hizo alizozungumzia kwenye Kanisa la Korintho, pamoja na suluhisho ambalo aliwapatia, tunaweza kupokea mwangaza wa jinsi tunavyoweza kukabiliana nazo ikiwa zatatukumba katika karne hii ya ishirini na moja.

Shida Paulo Alizofahamishwa Na Kloe

Shida alizofahamishwa na Kloe zilikuwa fitina katika Kanisa, zinaa, na hali kuwa Kanisa la Korintho lilikuwa likihusika katika mashtaka mahakama ya dunia huko Korintho.

Paulo alitoa mfano bora kwa wahudumu wa Makanisa alipowaambia jinsi alivyopokea habari za Kanisa lao. Katika (**1:11**), tunasoma, *'kwa maana, ndugu zangu, nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu.'* Kwa kutaja Kloe (Kanisa) – kundi la waumini waliokutana kwenye nyumba ya Kloe – kama chanzo cha shina la habari, Paulo alikuwa akionyesha kuwa hataki watu wajitambulishe wanapotoa habari kuhusu watu wengine katika Kanisa.

Wachungaji mara kwa mara huwa wanakumbana na washiriki wa Makanisa ambao hutaka kuwaeleza kuhusu 'mume au mke fulani wa fulani,' kwa masharti kuwa mchungaji hataelezea jinsi alivyopokea habari hiyo. Paulo hakuruhusu jambo hilo. Pia, alikuwa akionyesha kwamba hakuwa akifanya mashtaka yasiyokuwa na msingi kinyume cha baadhi ya washiriki wa Kanisa ila alikuwa tayari kuwashtumu na kuwarekebisha pamoja na kutenda jambo fulani la maana katika utatuzi wa matatizo hayo. Wakati washiriki wa Kanisa hawana uhuru wa kutoa majina yao ili kuthibitisha habari wanazotoa, ni wazi kwamba Paulo aliwachukulia kuwa watu wenye fitina- naye hawapa sikio.

Shida Za Migawanyiko Kanisani (Sura Ya Kwanza Hadi Ya Nne)

Washiriki wa Kanisa la Korintho walikuwa wamegawanyika kwa kuwa walikuwa wamefanyika wafuasi sugu wa wachungaji waliowapenda na kukataa kutambua viongozi na wachungaji wengine katika Kanisa. Paulo alikuwa mchungaji mwanzilishi na alikuwa amelisimamia Kanisa hili kwa miezi kumi na nane ya kwanza. Alitambulikana kama mmoja wa watu wenye elimu kuu siku zake. Na jambo hili liliwafanya baadhi ya Wakorintho kumtenga na kumfanya kuwa kiongozi wao wa kweli kwa kuwa mji huo wa Korintho uliwakilisha hali na kiwango kikuu cha elimu. Kanisa la Korintho lilikuwa kama Kanisa katika ustaraabu wetu katika mji ambao chuo kikuu.

Mtu mwingine kwa jina Apolo, alikuwa mhubiri mwenye ufasaha mwingi. Pia, alikuwa mhubiri huko Korintho. Ufasaha wake wa maneno uliwavutia wanafunzi wengi kwenye Kanisa hilo la kwanza la Korintho. Usemi wa, 'kuzungumza jinsi walivyozungumza katika Korintho,' unazungumzia kuhusu thamani isiyokuwa ya kweli iliyowekwa juu ya ufasaha wa unenaji kutoka kwa ustaarabu wa Wayunani/Wakorintho.

Wale waliokuwa hawana elimu kuu katika Kanisa hilo, kwa upande mwingine, walimkuza mtume Petro na kumweka katika daraja la juu. Haya mapendeleo kati ya waumini, yalisababisha mgawanyiko huo ambao Paulo alikuwa akizungumzia kwenye sura nne za waraka huu.

Shida La Zinaa Katika Kanisa (Sura Ya Tano)

Yamkini kuna mtu katika Kanisa hili la Korintho aliyekuwa akiishi pamoja na mke wa babake. Ingawa watu mle Kanisani walifahamu jambo hili, hawakutenda lo lote kumshauri mwenye mzinifu huyo. Paulo aliwakaripia waumini kuhusu tendo hilo la kutohusika katika sura ya tano, huku kwa ujasiri mwingi akiwaagiza kumwondoa katika ushirika wa Kanisa. Waraka wa pili wa Paulo kwa Wakorintho unathibitisha kweli kwamba waumini hao walifuata maagizo ya Paulo kumpokea mtu huyo katika ushirika wao tena (**2 Wakorintho 2:4-8**).

Shida Ya Waumini Kushitaki Wenzao (Sura Ya Sita)

Ingawa wanafunzi wa Kristo wana ubishi, Paulo aliwakemea kwa nguvu Wakorintho kwa kupeleka malalamishi yao mbele ya mahakama ya wasio haki, wala si mbele ya watakatifu. Hoja ya Paulo ilikuwa Roho Mtakatifu, ambaye anaishi ndani yao,

angeweza kuwasaidia kutatua ubishi wao. Kwa mafumbo, Paulo anamtaja aliye mnyonge miongoni mwao, ambaye Roho Mtakatifu anaishi ndani yake, kuwa amehitimu zaidi katika kushughulikia ubishi wao badala ya mahakama ya wasio haki. Paulo kwa hakika, hamaanishi hivi. Anatumia ucheshi na fumbo ili kuwaeleza jambo hilo. Anawaambia waumini hawa kuwa ni vyema kupoteza kuliko kumshitaki muumini mahakamani na kutatiza ushahidi wa Kristo katika jamii yao.

Mwongozo wake ambao umevuviwa umeizoa kile kinachojulikana kama *'Canon Law'* (sheria iliyokubalika) katika Kanisa la 'Warumi wa Katoliki.' Mwongozo huu pia umewafanya waumini wengi kukataa kutatua ubishi wao katika mahakama za 'wasio haki,' hata kama mtu atapoteza kitu anacho thamini sana. Waumini pia, wanatujulisha sura hii kwa kuuliza wosia kutoka kwa viongozi waliokomaa.

Maswali Wakorintho Waliyouliza Paulo

Maswali Kuhusu Ndoa (Sura Ya Saba)

Paulo anaanza sura ya saba ya waraka huu hivi, 'Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika,' Hii inadhihirisha chanzo cha pili cha Paulo wakati anapoandika na kuzungmuzia matatizo yaliyo katika Kanisa la Korintho. Tatizo la kwanza katika waraka huu ambao Kanisa hili lilimtumia Paulo lilizoa maswali kuhusu ndoa. Sura hii kuu kuhusu ndoa ndio jibu la Paulo kwa maswali ambayo Kanisa hili lilimuuliza.

Tafsiri jipya za Biblia zinaigawanya sura hii katika vifungu kadhaa. Kila moja ya vifungu kinawakilisha jibu la Paulo kwa swali kuhusu ndoa ambalo Kanisa lilimwuliza katika waraka wa Paulo. Kwa uangalifu mwingi, jibu linaweza kutambua swali lao lilikuwa lipi. Majibu ya Paulo yanastahili kufahamika kwa mtazamo bora wa mstari wa ishirini na sita unaosema, 'Kwa ajili ya shida iliyopo.' Shida iliyokuwepo ni mateso. Mengi yake mashauri ya Paulo katika sura hii yanafaa kutekelezwa wakati Kanisa linapokumbwa na shida ya mateso. Baada ya hayo kutendeka, ni vyema mwanamume asimguse mwanamke.

Pamoja na shida hiyo, Paulo alidhibitisha wale ambao hawajaolewa au kuoa bado wana weza kujitolea zaidi katika kazi za Bwana, ilhali wale ambao tayari wameoa ni lazima

washughulikie mambo ya wenzio. Katika vifungu vya kumalizia sura hii, Paulo kwa uakika, anafunza hali ya kuishi bila kuoa au kuolewa. Anaitaja hali hii kuwa karama.

Hata hivyo, Paulo aliwahimiza waumini kusheleka, kwamba wao wameoana au kwamba hawajaona kuliko kutawaliwa na tamaa katika maisha yao. Pia, alithibitisha kuwepo kwa ndoa kwa wale hawana mwito kuishi bila kuoa.

Ndugu Aliye Mnyonge (Sura Ya Nane Hadi Kumi)

Wengi miongoni mwa waumini wa Korintho walitaka kujua ikiwa ilikuwa vyema au vibaya kula chakula kilichotolewa sadaka kwa miungu. Paulo alizungumzia jambo hili kati ya sura za **8-10** za waraka huu. Alikusudia kwamba waumini wasile chakula kilichotelewa dhabihu kwa miungu ikiwa kitawakwaza waumini wengine. Hata hivyo, alielezea wazi kuwa kula chakula kilichotolewa kwa miungu kama dhabihu si najisi wala kutilia shaka imani ya mtu kwa kuwa katika yote, *'twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu*. (**8:4**).'

Sehemu kuu katika suluhisho la Paulo kwa tatizo hili ni wakati anapoendelea kuandika: 'Lakini angalieni hu uwezo wenu usije ukakwanza wale walio dhaifu. Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! dhamira yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu?

Alimalizia sehemu hii ya waraka huu kwa kushiriki kanuni tatu ambazo zinahitajika kutumiwa na kutekelezwa katika sehemu zinazotajwa kama za 'kijivu' kwenye utakaso. Namaanisha – mambo yale hayamo dhahiri kwenye Maandiko ambayo ni lazima kwetu kutenda, au kutotenda kama waumini ambao wameitwa na kutengwa kwa ajili ya kristo. Kanuni hizo tatu ni:

1. Fanya kila jambo kwa ukutufu wa Mungu.
2. Fanya mambo yale ambayo yataleta wokovu kwa ndugu mdhaifu aliyepotea.
3. Hakikisha kuwa hauitafuti faida yako mwenyewe.

Wajibu Wa Wanawake Kanisani (Sura Ya Kumi Na Moja)

Katika sura ya **11:10-2,** Pualo anazungumzia kuhusu sehemu ambayo wanawake wanashikilia pamoja na wanaume na Mungu. Kando na kuwahimiza wanawake kujifunika vichwa vyao wakati wanapoomba na kutoa unabii, pamoja na kuwashurutisha waume kuacha vichwa vyao wazi, Paulo anathibitisha kwamba wanawake huomba na kutabiri wakati Kanisa linapokusanyika.

Kifungu hiki hakiwashauri wanawake kuvaa kofia wanapokuja Kanisani. Hii ni kuhusu desturi na mila kuwa wanawake walikuwa wakivaa mavazi kwa mfano wa bui bui jinsi ilivyo hata sasa. Wakati yule mwanamke muumini alipoamua kwamba hatavalia mavazi ya kujisetiri kote mwilini, Paulo anaonya kwamba huwa hamheshimu mumewe. Sababu nyingine katika desturi na mila ile ni makahaba ambao walikuwa hawavai mavazi yenye kusetiri mwili kote na kuwa walikuwa wamefupisha nywele zao. Hii ndio sababu Paulo anaandika, ikiwa ni aibu kulingana na (desturi yako) kwa mwanamke kuiweka nywele fupi, basi nywele zake zahitajika kurefushwa. Ni dhahiri, kwamba hii inamaanisha ikiwa hakuna desturi sawa na hii, mwanamke mcha Mungu anaweza kuwa na nywele yake fupi.

Paulo anamalizia kwa kusema '*lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni Mungu* **(1 Wakorintho 11:3).'**

Kutia Najisi Meza Ya Bwana (Sura Ya Kumi Na Moja)

Katika sura ya **11: 23-34**, Paulo aliwakumbusha waumini wa Korintho umuhimu wa Meza ya Bwana (Ushirika Mtakatifu). Alitilia mkazo hali ya matayarisho yenye heshima kuu katika kutayarisha mioyo ambayo inahitaji kutangulia na kukumbatia Meza ya Bwana. Paulo aliandika kwamba waumini wanahitaji kushiriki katika Meza ya Bwana baada ya kujichunguza wenyewe na kwa njia inayostahili. Kwa sababu anaandika kwamba kushiriki katika Meza kwa njia isiyostahili kunaweza kuleta matokeo mabaya, wengi hujifikiria kuwa hawastahili kushiriki katika Meza hii. Tafsiri na utekelezaji unaokubalika ni kwamba, Paulo anawaonya Wakorintho wasije wakashiriki katika Meza 'Kwa njia isiyostahili.'

Sehemu ya Ujenzi Ya Waraka (1 Wakorintho 12-16)

Sura nne za mwisho ndio sehemu zenye ujenzi katika waraka huu. Sura hizi hutoa maagizo yenye suluhisho ya Paulo ambayo hueleza matatizo yaliyomo katika sehemu ya

urekebishaji katika waraka huu. Paulo anaanza sehemu hii hivi, ‘basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu.’ Mambo ya kiroho ambayo anawaagiza hapa ni: Karama za roho; maisha na uzima wa mwili wa Kanisa; Upendo; wajibu wa Kanisa linapokusanyika pamoja; utekelezaji wa ufufuo na utumishi wenye uaminifu.

Sura ya –**11:1** inaelezea jinsi Paulo alivyokumbana na matatizo katika Kanisa la Wakorintho. Ingawa walikuwa waumini na watu waliojawa na Roho Mtakatifu, walikuwa wangali wakihusika katika anasa nyingi za kimwili pamoja na mabishano. Paulo aliandika sura ya **12-16** kama suluhisho la kujumuisha katika matatizo yaliyokuwepo Kanisani. Alianza sehemu hii kwa kusema, ‘*Basi ndugu zangu, kwa habari ya karama za kiroho, sitaki mkose kufahamu* (**12:1**).’

Katika sura ya pili na ya tatu, Paulo aligawanya jamii ya binadamu katika sehemu tatu: Ya mtu wa kawaida (asiye wa kiroho), mtu wa kiroho na mtu wa kimwili. Mtu asiye wa kiroho (wa kawaida) hana Roho Mtakatifu. Mtu wa kiroho amempokea Roho Mtakatifu na pia anakaa ndani yake. Naye mtu wa kimwili amempokea Roho Mtakatifu ila amechagua kutembea katika ‘mwili,’ ambao Paulo anamaanisha ni, ‘asili ya utu wa kibinadamu ambao haina usaidizi kutoka kwa Mungu.’

Kutokana na mpangilio wa waraka wa Paulo, twaweza kutambua utu wa kiroho wa waamini wa Korintho. Paulo anawazungumzia kama ‘waliotakaswa.’ Baadaye, anawajata kama watu wa ‘kimwili.’ Unapofika katika sura ya kumi na mbili, unamsikia Paulo akisema, ‘Nisingeliwataka ninyi kubaki katika giza.’ Ni lazima tukubaliane kwamba waumini wa Korintho walikuwa watu wa kiroho, ila tabia yao ilikuwa ya kimwili kwani walikuwa hawana <u>ufahamu</u> wa watu wa kiroho.

Kulingana na Paulo, suluhisho la kiroho kwa matatizo yaliyokuwepo katika Kanisa lao lilianza kwenye wajibu wa Roho Mtakatifu (**Sura 12-16**). Roho Mtakatifu alikuwa amewapa karama za roho. Paulo alitaka kuwafunza hawa waumini kuhusu karama hiyo ili wakapate ufahamu zaidi jinsi Roho Mtakatifu alivyotaka kutenda kazi miongoni mwao kama Kanisa la Kristo aliyefufuka.

Upendo

Kwa kumaliza sura ya **12**, Paulo aliwaambia, *'Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora* (**31**).' Paulo aliendelea kuwapa kile kinachofahamika kama 'sura ya upendo katika Biblia (**1 Wakorintho 13**).' Sura hii kuu inatilia mkazo sifa kumi na tano ambazo hueleza hali ya utu wa upendo (**4-7**). Tunapo kifahamu kifurushi hiki cha sifa ambazo hudhihirisha upendo ambao ni tunda (thibitisho) la Roho Mtakatifu anayeishi ndani ya muumini, basi tunafahamu ukuu wa upendo miongoni mwa karama zile zingine za Roho mtakatifu (**Wagalatia 5:22,23**).

Upendo ndio 'njia iliyo bora' ambayo Roho Mtakatifu hutumia ili kusuluhisha matatizo maishani mwa waumini. Paulo alitumia fafanuzi hili lake la upendo ili kuwaonyesha Wakorintho jinsi ya kutatua matatizo Kanisani mwao.

Kufafanua hoja hii kuu ya waraka huu wa Paulo: Alifundisha kwamba Roho Mtakatifu hufanya kazi ya muujiza ndani ya muumini na thibitisho la muujiza huo ni upendo. Roho Mtakatifu hufanya muujiza mwingine wakati anapokuja juu ya muumini, au anapomtia mafuta muumini kwa ajili ya huduma. Thibitisho au ishara ya muujiza huo ni karama za Roho Mtakatifu ambazo humpa uwezo wa huduma hiyo. Hakuna kitu kama huduma ya muujiza ya Roho Mtakatifu juu ya muumini bila huduma ya kimiujiza ya Roho Mtakatifu ndani yake.

Uhai Wa Mwili

Katika sura ya kumi na mbili, Paulo alieleza Kanisa kuwa kama mwili. Katika sura ya kumi na nne, Paulo anaeleza utaratibu unaohitajika kunawiri miongoni mwetu wakati Roho Mtakatifu anapotenda miujiza yake ndani na juu yetu. Sura hii inafahamika kama 'sura ya ndimi' kwa kuwa Paulo anatoa mwongozo ulio dhahiri kulingana na karama ya ndimi na kutaja ndimi yamkini mara kumi na saba katika sura hii. Hata hivyo, hoja kuu katika sura hii ni jibu la Paulo kwa swali hili: *'Basi, ndugu, imekuawaje? Mkutanapo pamoja?* (**1 Wakorintho 14:26**).' Paulo hujibu swali hili kwa kusema jinsi inavyostahili wakati mwili wakusanyika pamoja. Zaidi ya mara arobaini katika sura hii, Paulo anatilia mkazo dhana kwamba waumini wanahitaji kujengana mmoja kwa mwingine wakati wanapokusanyika pamoja.

Ufufuo Uliotekelezwa (Sura Ya 15)

Ufufuo unamaanisha ‘ushindi juu ya kifo.’ Maanake ni zaidi ya ufufuo wa kimwili wa Kristo au yule Mkristo aliyeaga dunia. Katika sura hii ya ufufuo, Paulo anafunza kwamba ufufuo pia ni uwezo unaoendelea katika maisha ya kila siku ya muumini. La ziada ni kwamba, ufufuo wa Kristo ndio msingi wa imani yetu, kwa kuwa, ‘*Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu* (**15:17**).’

Ufufuo pia ni sehemu muhimu la Injili. Katika sura ya 2, Paulo aliwaambia waumini hawa kwamba alipokuja huko Korintho, hakunuia kujua jambo lingine ila tu Yesu Kristo na kusulubiwa kwake. Anamalizia waraka huu jinsi alivyoanza kwa kuwakumbusha Wakorintho kuhusu Injili aliyohubiri huko Korintho. Injili hiyo ni kweli mbili kuhusu Yesu Kristo: Kifo cha Yesu Kristo na Ufufuo Wake. Mistari ya kwanza minne kwenye sura hii ni usemi dhahiri wa Injili katika Agano Jipya. Punde tu Paulo anapoitaja Injili, anaandika mistari hamsini na nne kuhusu kweli ya pili ya Injili: Ufufuo wa Yesu Kristo.

Utekelezaji Wa Uwakili (Sura Ya 16)

Katika sura ya mwisho ya waraka huu, Paulo anazungumzia kuhusu kitu cha tatu cha roho ambacho anataka kushiriki pamoja na Wakorintho hawa. Anazungumzia kuhusu matoleo, au kwa ufasaha zaidi, uwakili wa Kikristo. Paulo alikuwa na mzigo mkuu kuhusu jambo hili kuhusu matoleo kwa kuwa alikuwa akiwauliza waumini wa mataifa kwenye Kanisa alizoanzisha kujitolea kabisa na kutoa matoleo kwa waumini wa Kiyahudi huko Yerusalemu na Uyahudi ambao walikuwa kwenye dhiki kutokana na janga kuu la njaa na mateso. Je! Si ni muujiza wa kuvutia sana kujua kwamba Sauli wa Tarso, ambaye alikuwa mtesi wa Wayahudi huko Uyahudi, kwa rehema nyingi anaomba matoleo watu wa mataifa kwa niaba ya wafuasi wa Kiyahudi wa Kristo ambao hapo mwanzoni, alikuwa akitia gerezani hata kuwaua. Hii kwa hakika ni dhihirisho la utu wa mwili wa Kristo ulimwenguni kote na jinsi washiriki wake wanavyoweza kusaidia kuleta uponyaji kwa kila mtu kupitia utekelezaji wa kanuni za uwakili mwaminifu.

Paulo Mchungaji

Paulo alihesabu utumzi wa uchungaji kwa Makanisa aliyoanzisha kama baadhi ya mateso yake. ‘*Baghairi ya mambo ya nje, yako yanijiayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote* (**2 Wakorintho 11:28**).’ Alikuwa tayari kuhatarisha yote aliyokuwa nayo

kwa ajili ya Makanisa yaliyokuwepo chini yake. Paulo alikuwa tayari kuudhiwa na hata kufa kwa ajili ya kukua kwao katika maarifa na ufahamu wa Kristo.

Kama matokeo ya moja kwa moja ya juhudi zake kwa Makanisa aliyoazisha, tuna lulu zenye kuvutia sana za nyaraka zake za uchungaji ambazo kwa sasa, zinatupa mwongozo wa njia ambayo twahitaji kujali Makanisa yetu. Kwa kuwa Makanisa yetu hukumbana na matatizo mengi ambayo katika siku za Paulo, walikumbana nayo, kwa kuwa aliyazungumzia katika nyaraka zake kama kwa Wakorintho. Tunajifunza kutoka nyaraka hizi jinsi tunavyostahili kujali na kuwakumbatia wale walio katika maangalizi yetu.

Ukaribu Wa Waraka Wa kwanza Wa Paulo Kwa Wakorintho

SURA YA PILI

Je! Kristo Amegawanyika (1 Wakorintho 1-4)

Wakorintho wa kwanza ni waraka wa kurekebisha ambao mchungaji mkuu na mwanzilishi yaani Paulo alikabiliana na shida katika Kanisa la Korintho. Shida ya kwanza ambalo Paulo alikumbana nayo ilikuwa mgawanyiko. Waumini walikuwa wamegawanyika kuhusu ni nani aliyekuwa kiongozi mkuu wa Kanisa lao. Maini yao juu ya viongozi kwa sehemu kuu, yalitegemea yule aliyewaongoza hadi kwa Kristo au aliyewabatiza. Maana yangu ni hii, ya kwamba wa kwenu kusema, *Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo* (**1:12**).' Lakini Paulo alikambiliana na tatizo hili la mgawanyiko kwa kuwauliza swali hii la kimsingi: 'Je! Kristo amegawanyika? (**13**).'

Wakati Paulo alipouliza kana kwamba Kristo alikuwa amegawanyika, alikwenda moja kwa moja hadi kwenye kina cha yale yaliyozunguka mgawanyiko uhuwa wa Kanisa la Korintho. Kwa msingi, kwa kuwa tunaamini ufufuo wa Kristo, pia tunamini Yesu Kristo yu hai na anaishi mioyoni mwetu.

Ikiwa Kristo anaishi mioyoni mwa waumini wote, basi wanahitaji kupatana katika mambo ya kimsingi kuhusu Kristo na kufahamu kwamba Kristo hawezi kugawanyika katika mambo haya. Je! Kristo anayeishi ndani yetu huhisi ukabila au ubanguzi rangi kwa njia gani? Ikiwa Kristo anaishi ndani yetu, nasi tunaishi ndani Yake, twahitajika kuhisi vipi kuhusu ukabila au mambo mengine?

Ikiwa ubaguzi wa rangi au ukabila au adhabu ya kifo, ungeibuka miongoni mwetu, kwa sababu Kristo anayeishi ndani mwetu hujihisi kwa njia moja tu kuhusu mambo haya, basi twafahamu kwamba tatizo letu la migawanyiko kuhusu mambo hayo sio kwa sababu Kristo huhisi mambo mengi kuhusu mambo hayo. Tatizo la migawanyiko yetu ni kwa sababu ya mambo hayo ndani yetu, sisi wafuasi Wake. Makosa yanahitaji kupatikana ndani yetu. Paulo alikuwa akiandika ili kurekebisha makosa ya migawanyiko miongoni mwa Wakorintho huku akitoa ujumbe muhimu wamfuate Kristo wala si viongozi wa kibinadamu. Aliwaandikia wale waliokuwa wakiandamana naye katika huduma yake ya sura nne katika waraka wake wa kwanza.

Anamalizia sehemu hiyo kwa kuandika kwamba ndiye alieipanda Kanisa, naye Apolo akalimwagia maji, ilhali Mungu akaikuza. Anaendelea kutangaza kwamba pamoja na yule aliyeimwagilia maji, wao si kitu kwani ni Mungu aliyeifanya kukua. Hivyo basi, hatustahili kujikuza katika wanadamu, bali 'Yeye ajikuzaye, ajikuze kwake Bwana.'

Usitukuze Ubatizo

Paulo alianza ujumbe wake kinyume cha mgawanyiko kwa kusema, '*Maana Kristo hakunituma ili niwabatize, bali niihubiri Habari Njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika* (**1:17**).' Tangazo la Paulo hapa linaleta utofauti kati ya umuhimu wa ubatizo na wa kuhubiri Injili.

Huku waumini wakiendelea kwenye hoja kuhusu jinsi ubatizo unavyohusika na wokovu, ujumbe wa Paulo unatufunza kwamba ubatizo hautuokoi. Na ikiwa ungeliweza, basi angeuongeza katika ujumbe wa Injili yake badala ya kuuweka miongoni mwa jambo ambalo hakutaka kutenda. Anaandika kuwa kama angewabatiza waumini wengi wa Korintho, wale aliokuwa amewabatiza wangemfuata badala ya kumfuata Kristo.

Usitukuze Hekima Ya Ulimwengu

Paulo aliuliza, '*Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mleta hoja za zamani hizi? Je Mungu hakuifanya hekima yake, ya dunia kuwa ni upumbavu?….mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichangua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu* (**1:20, 27**).'

Raia wa Korintho walisifika sana kwa hoja zao zilizokuwa barazani, na kutilia mkazo elimu na filosofia. Watu hawa wenye elimu na uwezo mkuu walijitambua kuwa bora kuliko wale hawakuwa na ufasaha wa maneno au elimu.

Lakini Paulo alitoa ujumbe tofauti huko Korintho. Aliwafunza waumini hao wa Korintho kwamba wenye hekima katika ulimwengu huu hawana na hekima machoni pa Mungu. Badala yake, Mungu huwatumia wanaotambulika kama wapumbavu ili kuwaaibisha wenye hekima, ili utukufu wake upate kufunuliwa. Hali hii haimaanishi kuwa haiwezekani wenye elimu kumfahamu Mungu, au ni wapumbavu tu walio na uwezo wa kumfahamu. Bali inamaanisha kwamba kujisifu kwako kunahitaji kuwa kwa Mungu wala sio kwa ajili yetu wenyewe: *'Kwa tendo lake mko ndani ya Kristo Yesu, ambaye amefanyika kwetu hekima kutoka kwa Mungu, na haki na utakaso, pamoja na ukombozi, ili kwamba, kama vile ilivyoandikwa, 'Yeye ajisifuye, ajisifu katika Bwana (***4:30**).'

Usitukuze Mhudumu

Huku akiendelea katika ujumbe wake, Paulo alidhihirisha kwamba Roho Mtakatifu peke yake ndiye chombo kinachotoa uhai katika uzao wa kiroho: *'Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa. Nami nalikuweko kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika nguvu za Mungu* (**2:1-5**).'

Mungu huwatumia wanadamu ili kuwasilisha ujumbe Wake wa wokovu, lakini humtumia Roho Mtakatifu ili kutabua mabadiliko ndani mwa wale wanaosikiliza Injili. Mabadiliko ya kiroho hayatokani na ufasaha wetu wanadamu bali kwa uwezo wa Roho Mtakatifu anapotembea ndani ya wale wanaoisikiliza Injili. Kwa kuwa Paulo alikuwa akiwazungumzia Wakorintho waliokuwa wakimpendelea pamoja na uongozi wake, aliwahimiza kwa ufasaha wasimtukuze katika uwezo wake au kutokana na karama yake. Wakati alipoandika sura hizi nne za kwanza za waraka wake kwa Wakorintho, ni dhahiri

alikuwa akiwaelekeza kujitukuza katika nguvu za Roho Mtakatifu ambaye alikuwa amewaokoa wakati walipomsikia akiihubiri Injili katika mji wa Korintho.

Mtukuze Roho Mtakatifu Kama Mwalimu Wako

Tunaposoma kitabu, huwa tunajifunza kwa macho yetu wenyewe. Tunaposikiliza hotuba, huwa tunajifunza kwa masikio yetu. Tunapotumia yote pamoja, huwa tunajifunza zaidi jinsi tunavyofaidika kutokana na kujifunza kwa vyombo vya sauti na picha. Tunaweza kujifunza kupitia hisia zetu, na kwa hiari yetu wenyewe, au kupitia moyo wetu. Lakini Paulo aliwafunza Wakorintho hawa kwamba wangejifunza elimu ya kiroho kupitia Roho Mtakatifu: *'…Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu* **(2:9-10).'**

Paulo alifunza kwamba Roho wa Mungu peke yake hufunza mambo ya kiroho kwa mwanadamu. Mwanadamu hawezi kujifunza kweli ya kiroho kupitia macho, au masikio yake au moyo wake tu. Kulingana naye, ni lazima mwanadamu ajifunze kweli ya kiroho kupitia Roho Mtakatifu.

Mtu wa kiroho amempokea Roho wa Mungu, naye Huyu Roho humpa uwezo wa kujua na kufahamu nia ya Mungu. Paulo aliutumia mfano wenye kushangaza ili kueleza sehemu hii ya mwisho: *'Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu* (**11-12).'**

Mtu anayefahamu kile mwenzake anawazia ni roho wa mtu huyo. Kwa njia hiyo, roho peke yake anayefahamu kile Mungu anachiowazia ni Roho wa Mungu. Kwa kuwa tumepewa Roho wa Mungu, twaweza kufahamu mawazo ya Mungu.

Mtu wa tabia ya asili, kwa upande mwingine, hawezi kuelewa mambo yaliyo ya roho: *'Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake*

huyu ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni (**14**).’ Mtu wa tabia ya asili hawezi kuelelewa mambo ya roho, kulingana na Paulo.

Mtukuze Mungu Kama Kiongozi Wako

Katika sura ya tatu, Paulo aliwaambia Wakorintho kwamba walikuwa na tabia ya watu wasio wa roho. Ingawa alikuwa amewatambua kama waumini waliotakaswa hapo mwanzoni mwa waraka wake, pia aliwatambua kama waliokuwa mbali na mahali walimohitajika kuwepo, huku akiwataja kama ‘*watoto wachanga katika Kristo’* na ‘*wa kimwili* (**1,3**).’ Migawanyiko yao ilithihirisha kweli kwamba walikuwa watu wa kimwili, au walikuwa na tabia ya kimwili: ‘*Maana ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?* (**3**).’ Jinsi walivyokuwa wamegawanyika na kuwazunguka viongozi wao kuonyesha kwamba walikuwa watoto wachanga kiroho na nia yao kwa viongozi ilikuwa ni ya kitoto.

Badala yao kugawanyika kuhusu sifa za viongozi wao, walihitaji kufahamu wajibu ambao Mungu anautenda hatimaye kama kilele na kichwa cha mwili wao: ‘*Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye* (**5-7**).’ Tena, ujumbe wa Paulo ulikuwa wao wamfuate Mungu, wala si wanadamu, naye akamaliza sehemu hii kwa kusema, ‘*Basi, mtu ye yote na asijisifie wanadamu* (**21**).’ Usijisifie wanadamu wala usiwafuate. Jisifie Mungu na umfuate, kwa kuwa ni Yeye amewachagua wanyonge na wapumbavu katika ulimwengu huu ili awaibishe wenye nguvu.

SURA YA TATU

Upendo Unaotatanisha

Jinsi Paulo alivyokuwa akiwaambia Wakorintho wasigawanyike miongoni mwa viongozi wao, aliongezea funzo kuhusu hukumu: ‘*Lakini, kwangu mimi, si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu. Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa ajili hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana. Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu* **(4:3-5**).’

Kuhukumu Moyo Wa Mwanadamu . . .

Wengi miongoni mwa Wakorintho walikuwa wakimhukumu vyema Paulo, juu ya viongozi wengine Kanisani. Lakini Paulo aliwaeleza kwamba hukumu yao yenye kumpendelea haikumaanisha cho chote kwa kuwa haikumfanya kujihisi kwamba alifaulu kujihukumu, bali na kuikubali hukumu waliokuwa nayo wanadamu kwake. Alihisi hawezi kuhukumu nia zilizokuwepo ndani ya moyo wake, naye akaunyosha upungufu wake kwa wanadamu wote. Kwa sababu moyo wa mwanadamu ni wenye kina kikuu kuliko ufahamu wake mwenyewe, Paulo alifunza kwamba twahitaji kumwachia Mungu hukumu ya mioyo ya wanadamu.

Kuhukumu Matendo Ya Mwanadamu . . .

Kwa sababu hatufahamu nia zilio mioyoni mwetu, je! Tunawezaje kufahamu nia zilizo ndani ya mioyo ya wengine? Huku Paulo akitupa mwongozo tusihukumu nia ya wengine, funzo hilo halimaanishi kwamba tusiwahukumu wengine. Hiyo inahusu hukumu yetu kwa nia zilio mioyoni mwa watu wengine.

Kwenye sura inayofuata ya waraka huu (s**ura ya 5**), Paulo aliwakemea watu hao kwa kutohukumu mtu ambaye walistahili kuhukumu – mtu ambaye alikuwa akiishi na mke wa babake mzazi katika hali ya zinaa. Paulo anawakemea Wakorintho hawa kwa kuwa hawakuhukumu mtu huyo. Alisema: *'Naliwaandikia katika waraka wangu, kwamba msichangamane na wazinzi. Sisemi msichangamane kabisa na wazinzi wa dunia hii, au na wenye kutamani, au na wanyang'anyi, au na wenye kuabudu sanamu; maana hapo ingewalazimu kutoka katika dunia. Lakini, mambo yalivyo, naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye. Maana yanihusu nini kuwahukumu wale walio nje? Ninyi hamwahukumu hao walio ndani? Lakini hao walio nje Mungu atawahukumu. Ninyi mwondoeni yule mbaya miongoni mwenu* (**5:9-13**).'

Katika kifungu hiki, twajifunza kuwa hukumu inaweza kutumika kwa yule aliye ndani na hata aliye nje ya Kanisa. Hatustahili kuwahukumu walio nje au kujitenga nao kwa sababu ya matendo yao ya dhambi. Ikiwa tutatengana nao kabisa, kwa hakika hatutaweza kushiriki na katika Injili. Badala yake, ni lazima tachie Mungu hukumu ya wasioamini na

kuendelea kushiriki pamoja na katika neema itokayo kwa Kristo. Kuhusu walio ndani ya Kanisani, wale ambao hukiri kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani yao ili kuwafunza na kuongoza mapito ya hatua zao; ni lazima kukabiliana nao ikiwa matendo yao hayalingani na kile wanachodai kuamini. Hata hivyo, kuhusu mwenye zinaa ndani ya Kanisa, Paulo aliwaona waumini wa Korintho kutowajibika kwani hawakuhusika wala kuhukumu mtu huyo.

Kufahamu Wakati Wa Kukabiliana . . .

Ni dhahiri kwamba, Maandiko hayafunzi kwamba hatustahili kuhukumu wenzetu. Waumini wengi humnukuu Yesu kwa upendo tunapokabiliana nao. Wao husema, 'Yesu alisema, 'Usihukumu' Hayo ni baadhi ya maneno aliyosema Yesu kuhusu kuhukumu wengine. Kwa hakika, alizungumzia mengi kuhusu kuhukumu wengine baada ya kusema, 'Usiwahukumu wengine.' Yesu alifunza kwamba tusihukumu matendo ya mtu kwanza ikiwa hatujahukumu kwanza matendo yetu (**Mathayo 7:1-5**). Lakini zaidi ya hayo, ni wajibu wetu kama washiriki wa jamii ya Mungu kukabiliana na wale wanaojidhuru wenyewe au kuwadhuru wengine katika mwili wa Kristo (**Mathayo 18:15; Wagalatia 6:1**).

Wakati Paulo alipowahimiza waumini wa Korintho kukabiliana na yule mtu aliyekuwa akiishi katika dhambi, alilipima deni ya kukabiliana katika mwongozo fulani. Kwanza, yule mtu alidumu katika dhambi. Hii haikuwa dhambi ambayo mtu huyu alitenda mara moja tu kisha kutubu. Badala yake, alizidi kudumu katika dhambi hiyo na hapakuwa na ishara kuonyesha kuwa alikuwa tayari kuiacha. Ingawa hakuna dhambi ambayo inazidi wala kuzidi msamaha Wake, Mungu hawezi kumsemehe mtu ambaye anakataa kusamehewa au hataki kutubu dhambi yake. Kwa kuwa mtu huyu haonyesha dalili ya toba au kugeuzwa mwenendo wake, Paulo alishauri kwamba atengwe na mwili, ambayo ndio hatua ya pili yake katika sura ya tano ya waraka huu: Mwamini ambaye hataki kutubu dhambi ni lazima aondolewe katika mwili wa waumini.

Kuwa Na Hamu Au Nia Nzuri . . .

Hamu ya kukabiliana hutokana na upendo. Sisi hukabiliana na ndugu zetu ambao wanaishi katika dhambi kwa sababu tunawapenda kiasi kwamba hatuwezi kutulia na kutazama wakiendelea kuhatarisha uhusiano wao na Kristo na watu wengine. Lengo letu

katika kukabiliana ni kushuhudia mtu huyo akirejeshwa katika mwili wa Kristo, jinsi Maandiko ya (**Mathayo 18: na Wagalatia 6**) yanavyotufunza, kuwa Mungu huwarejesha *'kwa roho ya upole* (**Wagalatia 6:1**),' na '*kuwaongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake* (**Zaburi 23:3**).'

Kumkabili kaka au dada katika Bwana kwa sababu ya matendo yake inamwonyesha kuwa kuishi katika dhambi ni vigumu lakini muhimu. Mpango wetu katika kuwarejesha katika ushirika na Bwana pamoja na mwili wa Kristo ni kuwasaidia kufahamu hatari iliyopo katika matendo yao yalivyo kwa maisha yao wenyewe na katika uhusiano wao. Hii ni kweli hasa wakati dhambi ya uasherati inahusika.

Dhambi katika maisha ya muumini pia hugusia ushuhuda wao kwa wasioamini pamoja na ushuhuda wetu kwao. Wengi wa wasioamini hufikiria kwamba waumini wengi ni wanafiki. Wao wakimwona muumini akiishi katika dhambi, wanamtambua kama mnafiki na kuwa na sababu moja zaidi ya kukataa Injili pamoja na wokovu. Wanapoona tukishirikiana na muumini huyo na kutambua kuwa hakuna jambao linalotendaka kuhusu dhambi yake, wao pia hututambua kama wanafiki. Kwa ajili ya wema wa kiroho wa yule kaka au dada katika mwili wetu wa Kristo, na kwa ushuhuda wa kila muumini katika Kanisa letu; ni muhimu kwetu kukabiliana naye katika upendo na upole huku tukiweka kurejeshwa kwake katika Kristo na mwili mbele ya makusudio yetu kutenda hivyo.

SURA YA NNE
Mwongozo Wa Ndoa
(1 Wakorintho 7)

Sura ya saba ya Wakorintho wa kwanza imefahamika kama 'sura ya ndoa katika Biblia.' Inagusia maswali kadha ambayo washiriki wa Kanisa la Korintho waliyoweka mbele zake Paulo katika barua waliyomwandika kuhusu ndoa, kuishi pweke, talaka, kufanya ndoa mara ya pili na uhusiano wa kiroho katika ndoa. Kwa karne nyingi, wakati washiriki wa Kanisa walipowaendea wachungaji wao wakiwa na hoja kuhusu mambo haya ya ndoa, sura hii imekuwa kuwa mwongozo kuhusu ndoa kwa mchungaji.

Jambo la msingi ambalo linatiliwa maanani katika sura hii ni, ‘ndoa ni nini machoni pa Mungu?’ Maswali haya yote yanagusiwa katika sura ya saba ya Wakorintho wa kwanza, ambapo twavumbua mpango wa Mungu kwa ndoa na hali zote za shida ambazo zinaweza kuchibuka katika uhusiano wa ndoa.

Wengi hubishana kuwa sehemu nyingi katika sura hii hazijavuviwa kwa kuwa wakati mwingine, Paulo alizungumza kutokana na mamlaka ya Bwana ilhali mara kwa mara alitoa maoni yake mwenyewe katika mambo fulani. Kwa mfano, Paulo alithibitisha kwamba mafunzo yake yalikuwa yametoka kwa Bwana wakati alipowaambia, *‘Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe* (**10**).’ Hata hivyo, wakati mwingine, alifanya wazi kuwa mafunzo yake hayakuwa yametoka kwa Bwana ila yalikuwa maoni yake: *‘Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana; ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyu anakubali kukaa naye, asimwache. . . Kwa habari za wanawali sina amri ya Bwana, lakini natoa shauri langu, mimi niliyejaliwa kwa rehema za Bwana kuwa mwaminifu. . . Lakini heri yeye zaidi akikaa kama alivyo; ndivyo nionavyo mimi; nami nadhani ya kuwa mimi nina Roho wa Mungu* (**12, 25, 40**).’

Pamoja na maoni ya ‘kibinadamu’ ambayo Paulo alitoa kwenye mistari hii, hatuwezi kuhesabu maneno yake kuwa hayakuwa yamevuviwa au kutoka kwa Bwana. Paulo alikuwa mwangalifu katika sura hii kujenga juu ya mafunzo ya Kristo. Pale maswali haya yalipojibiwa katika mafunzo ya Yesu na sheria ya Mungu, Paulo alithibitisha na kunukuu kile Bwana alichofunza. Hata hivyo, pale Yesu au sheria ilikuwa kimya, alizungumza kama mtu ambaye *‘kwa rehema za Mungu angelitumainiwa.’* Maneno yake ya mwisho katika sura hii ya ndoa ni kwamba, ‘*alikuwa na Roho wa Mungu* (**25, 40**).’

Hakuna njia ye yote Paulo angeonyesha mawazo yake katika sura hii ya ndoa kwamba yalikuwa bado hayajavuviwa. Kwa maneno yake ya mwisho katika sura hii, alithibitisha kua yale aliyowaandikia Wakorintho kuhusu ndoa, yalikuwa yamevuviwa na Roho wa Mungu.

Kwa Hali Ya Dhiki Iliyopo Sasa . . .

Kote katika sura hii, Paulo anatilia mkazo ushauri kwamba Wakorintho wasifanye ndoa au kuitafuta hali nyingine tofauti kuliko ile waliokuwa wakiishi wakati walipoazimia kumfuata Kristo. Aliwashauri hivyo kwa sababu ya kile alichotaja kama '*shida iliyopo* (**26**).' Kanisa lilikuwa likiishi wakati wa mateso na kwa sababu hiyo, Paulo alifikiri ni bora ikiwa kwa kuwa hakuwa na mke kubaki vivyo hivyo badala ya kuzidisha fedheha katika maisha ya kila siku.

Ni dhahiri kwamba, katika barua yao kwake, walimwuliza ikiwa wana wao waliokuwa hawajaoana wakati huo wangeoana wakati huo mgumu. Paulo kwa uwazi kabisa aliwaambia kwamba wana wao wa kike walio wanawali pamoja na wa kiume wanastahili kuwa na hekima na kubakia walivyo. Hawakatazi vijana hawa kufunga ndoa, ila anawahimiza kuishi jinsi walivyo. Kwa sababu hii, aliazisha sura hii kwa kuwaambia, *'Ni vyema ikiwa mwanamume hatamgusa mwanamke* (**1**).' Ikiwa vijana hawa wangekubali kuishi peke yao bila kufunga ndoa, basi aliwashauri kujikinga na tamaa.

Ingawa Paulo alikuwa amewashauri wale waliokuwa bado kuoa kuishi jinsi walivyokuwa, pia alikubaliana nao kwamba kuchangua kufanya ndoa haikuwa (**9, 28, 36**).

Kuna maoni kuwa huenda Paulo alikuwa ameoana, kwani kama mshiriki wa baraza kuu la dini yaani *Sanhedrini,* alitarajiwa kuwa na mke. Hata hivyo, katika sehemu anayogusia kwa wale ambao bado hawajaoa na pia wajane, aliwashauri 'kubakia kama alivyokuwa.' Wasomi wengi hukubaliana kuwa alikuwa mjane.

'Msinyimane. . . .'

Uhusiano wa kimwili kati ya mke na mume kusudi lake ni kwa ajili ya uzazi na raha au ridhaa kwa wenzi wawili. Paulo aliunga mkono wazo hili kwa kuandika hivi*: 'Mume na ampe mkewe haki yake, na vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe. Msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu (**3-5**).'*

Mistari michache kabla ya kifungu hiki, Paulo alizungumzia watu waliokuwa hawajaoa bado kwa kusema, *'Ni vyema ikiwa mwanamume hatamgusa mwanamke'* (**1**),

lakini halihusiani na watu walio katika ndoa. Kulingana na kifungu hiki, ngono inastahili kuwajali-wengine na kwa ajili ya ridhaa yao. Mume anastahili kumfurahisha mkewe, ilhali mke pia anastahili kumfurahisha mumewe, kwa hivyo hawastahili kunyimana uhusiano huu wa karibu wa ngono.

Mipaka ya ngono iliyomo kwenye ndoa sio kuhusu lililo jema au baya, ililo la kawaida au lisilo la kawaida. Neno kuu ni ‘makubaliano.’ Cho chote kile waliooana wanachotenda ili kupeana raha hakikubaliwi wala hakikatazwi. Cha muhimu ni kwamba kuna makubaliano. Paulo alisema kwamba sababu ya kipekee mume au mke kutokuhusiana katika hali ya ngono ni wanapoutumia wakati wao kuomba na kufunga, na kwamba uamuzi huu unastahili kutokana na makubaliano kati yao wawili.

Hili halituonyeshi tu mpaka ya kutengana katika uhusiano wa kimwili, bali pia aina ya uhusiano wa kiroho ambao mume na mke wanashiriki. Ingawa wamo katika ndoa na kushiriki umoja wa kimwli mbele za Mungu, bado wangali na uhusiano wa kibinafsi na Mungu. Uhusiano ulio karibu sana katika maisha haya sio wa ndoa. Ni wetu na Mungu. Watu hushiriki uhusiano kuhusu ndoa zao kwa uhuru mwingi kuliko jinsi wanavyofanya na Mungu.

Kifungu hiki kinafunza kuwa njia bora kujikinga dhidi ya zinaa ya usherati kati ya wawili katika ndoa ni kutosheka na ushirika wo wa ngono katika mipaka ya ndoa. Mji wa Korintho ulikuwa umelowa katika zinaa, na Paulo aliwahimiza waliokuwa katika uhusiano wa ndoa kutosheleza mahitaji yao ya ngono katika mipaka ya nyumbani ili kujikinga na majaribu. Uhusiano wenye nguvu wa kutoshelezana ni kinga bora dhidi ya majaribu ya zinaa.

‘Mungu Ametuita Kwa Amani . . .’

Kando na kuishi na kuwa pweke katika uhusiano wa ndoa, sura hii pia inagusia mambo kuhusu talaka. Ni dhahiri kwamba Wakorintho walimwuliza Paulo katika barua yao ikiwa waumini wawili waliruhusiwa kutamatisha ndoa yao kwa talaka. Katika msitari wa **10 na 11,** Paulo alijibu swali lao. Kwa urahisi alijibu kwa kusema, ‘la Hasha.’ Alinukuu mafunzo ya Yesu kwa Wakorintho kuhusu kutovunja ndoa ambako Yesu alikuwa

amewaonyesha Mafarisayo, ambayo yalikuwa yameungwa mkono na sheria (**Mathayo19:3-9**).

Katika mistari ya **12-16**, Paulo alizungumzia swali ambalo halikuja moja kwa moja kutoka kwa Yesu: 'Je! Talaka yaruhusiwa kati ya asiye amini na anaye amini? Ushauri ambao Paulo alitoa kuhusu jambo hili ni wenye kukubalika*: 'Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana; ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye asimwache. Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye asimwache. . . Lakini yule asiyeamini akiondoka, na aondoke. Hapo huyo ndugu mume au ndugu mke hafungiki. Lakini Mungu ametuita katika amani. Kwa maana wajuaje, wewe mwanamke, kama utamwokoa mumeo? au wajuaje, wewe mwanamume, kama utamwokoa mkeo* (**12-13, 15-16**).'

Paulo aliwaambia Wakorintho kwamba mwenzi anayeamini anaweza kuishi pamoja na asiyeamini na kuwa mfano wa upendo wa Mungu pamoja na neema ili apate kuokolewa (t**azama 1 Petro 3: 6**). Ikiwa ndoa ingevunjwa, yule mwenzi asiyeamini ndiye angefanya uamuzi huo. Na ikiwa asiyeamini angetaka talaka, basi yule anayeamini anastahili kumwacha huru. Jambo hili linapotokea, ndugu huyo '*hafungiki* (**1 Wakorintho 7:15**).'

Kioo Chenye Pembe Tatu Cha Upendo

Wasomi bado hawajakubaliana kikamilifu kuhusu kile Paulo alichomaanisha kwa kuzungumzia kuhusu 'kufungwa' katika msitari wa **15**. Baadhi ya wasomi wanaamini kwamba muumini yuko huru kupokea talaka yake lakini hawezi kufunga ndoa nyingine ikiwa yule asiyeamini atajitenga na ndoa hiyo, kwa kuwa Maandiko yanazungumzia kuhusu kutoolewa ikiwa mwenzi wa kwanza yu ngali hai (**Warumi 7:2-3**). Wengi huamini maana yake ni kwamba, wanaweza kutalikiana na kuwaoza wake au waume wengine, kwani mstari huo unasema kwamba yule mwenzi yuko huru.

Ingawa wasomi hawakubaliani kuhusu tafsiri ya mstari huu, ni lazima tuutafsiri katika Roho wa Upendo. Kulingana na Paulo, Mungu alimpatia mwanadamu sheria kwani alimtaka aishi vyema, wala sio kwa sababu alitaka kumfunga. '*Nasema hayo niwafaidie; si kwamba niwategee tanzi, bali kwa ajili ya vile vipendezavyo, tena mpate kumhudumia Bwana pasipo kuvutwa na mambo mengine* (**1 Wakorintho 7:35**).'

Upinzani kati ya Yesu na Mafarisayo unaweza kuelezwa kwa njia hii: Kabla ya Yesu kuitekeleza sheria ya Mungu katika maisha ya watu, Aliipitisha kwenye kioo cha pembe tatu cha upendo wa Mungu. Mafarisayo bila huruma ‘walitupia watu kitabu.’ Hivyo basi, twahitajika kupitisha mafunzo ya sheria ya Mungu kwenye kioo cha pembe tatu cha upendo wa Mungu kabla ya kuitekeleza sheria Yake katika maisha ya watu.

Kwa mfano, tunaweza kushangaa ikiwa mtu ambaye alitalikiwa kabla ya kufanyika muumini anaweza kuruhusiwa kufunga ndoa tena ilhali Maandiko yanafunza kwamba mtu aliyetalikiwa haruhusiwi kufanya ndoa nyingine hadi aliyemtaliki atakapofariki. Ikiwa tungewaambia jambo hili, tungekuwa kama Mafarisayo ambao walitumia sheria iliyokusudiwa kudhihirisha upendo wa Mungu kwa wanadamu na kuyafanya maisha yao kukosa ladha ya sheria. Mafarisayo walifanya kitendo kama hiki kuhusu siku ya sabato kwa kumkemea Yesu baada ya kumponya mtu badala ya kutofanya cho chote, ilhali Yesu alipitisha sheria hiyo kwenye kioo cha Upendo wa Mungu. Baadaye, akawakemea wale Mafarisayo kwa kusema, ‘Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, wala sio mwanadamu kwa ajili ya sabato (**Marko 2:27**).’

Basi ni kwa sababu gani Mungu akafanya sheria za ndoa? Kwa kuwa alimtaka mwanamume na mwanamke alifunga ndoa aishi kwa baraka za ndoa na jamii. Mungu pia alitaka kuwa na mfumo ambao ndoa na jamii zingejimudu kwao. Lakini mara kwa mara sisi hutumia sheria hizo za ndoa kuwatenga watu mbali na maisha ya kutosheka ambayo Mungu alikukusudia alipotoa sheria za ndoa. Jinsi Paulo anavyosema, *‘kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha* (**2 Wakorintho 3:6**).’

Ikiwa una tafsiri ya Agano Jipya ambayo inagawa sura hii katika sehemu ndogo ndogo za vifungu, ikiwa utasoma kila kifungu, basi utatambua swali la Wakorintho lilikuwa lipi walilomwuliza Paulo katika waraka wao ambao alijibu katika kifungu hicho. Tunaweza kukubaliana kwamba Wakorintho waliuliza swali kuhusu talaka na kufanya ndoa kwa mara ya pili kati ya waumini; ndoa iliyochanganyika kati ya kaka au dada ambaye amefaamini ilhali mwenziwe hajaamini; na hivyo kujipata wakiwa wasioamini. Tena walitaka kujua ikiwa wanao ambao bado hawajafanya ndoa wanawqeza kufanya hivyo nyakati hizo za misuko-suko na mateso.

Ni dhahiri Wakorintho waliuliza kuhusu kile waumini wapya wanachotaka kutenda wale waliokuwa wameoana tena kabla ya kupokea wokovu. Tunaweza kusema kwamba Wakorintho hawa walikuwa wamemwuliza Paulo aina ya swali sawa na hilo kwa sababu ya kifungu moja katika sura hii (**17-24**). Tunaweza kufupisha jibu la Paulo hivi: Hatuhitaji kubadilisha matukio ya kale ya waumini wapya, kama kuwaeleza kuoa tena mtu waliyetalakiana katika ujana wao au kutalikiana na waume wao wa pili. Mara tatu katika kifungu hiki, Paulo alifunza hivi: *'Lakini kama Bwana alivyomgawia kila mtu, kama Mungu alivyomwita kila mtu, na aende vivyo hivyo. Ndivyo ninavyoagiza katika makanisa yote. . . Kila mtu na akae katika hali ile ile ambayo alikuwa nayo alipoitwa. . . Ndugu zangu, kila mtu na akae mbele za Mungu katika hali iyo hiyo aliyoitwa nayo (**17, 20, 24**).'*

Paulo alitumia neno 'kuitwa,' mara kadha katika waraka huu. Naye anapofanya hivyo, anazungumzia kuhusu wokovu wa watu ambao anawazungumzia. Wakati mwanamume au mwanamke anapopata wokovu, anahitajika kumwuliza Mungu aibariki ndoa yake ambayo amefunga. Na ikiwa yumo katika ndoa pamoja na asiyeamini anastahili kujilinganisha na mafunzo ya Paulo katika **7:12-16. Pia** ikiwa yuko katika ndoa, basi wanahitajika kumwuliza Mungu ikiwa anataka aishi pweke bila kufanya ndoa.

Useja: Kumtumikia Mungu Bila Kupotoshwa

Baadaye, Paulo aliorodhesha sifa za useja mwishoni mwa sura hii*: 'lakini nataka msiwe na masumbufu. Yeye asiyeoa hujishughulisha na mambo ya Bwana, ampendezeje Bwana; bali yeye aliyeoa hujishughulisha na mambo ya dunia hii, jinsi atakavyompendeza mkewe. Tena iko tofauti hii kati ya mke na mwanamwali. Yeye asiyeolewa hujishughulisha na mambo ya Bwana, apate kuwa mtakatifu mwili na roho. Lakini yeye aliyeolewa hujishughulisha na mambo ya dunia hii, jinsi atakavyompendeza mumewe. Nasema hayo niwafaidie; si kwamba niwategee tanzi, bali kwa ajili ya vile vipendezavyo, tena mpate kumhudumia Bwana pasipo kuvutwa na mambo mengine* (**32-35**).'

Paulo alifunza ili kumtumikia Mungu bila kupotoshwa unafaa kubaki katika hali ya useja. Mazungumzo hayahusiani na 'shida iliyopo' ambayo alizungumzia kwenye sura hii bali kwa mtazamo usio na mgawanyiko wa moyo wa mtu kwa Bwana. Ikiwa ni kujitolea kwa aina hiyo, ni vyema ikiwa mtu hataingia katika, ingawa uamuzi wake haumfanyi kuwa

duni dhidi ya yule aliye katika ndoa. Mwanamwali anayeingia katika ndoa atakuwa na wakati mgumu kugawanya kujitolea kwake kati ya mumewe na Bwana. Uamuzi wa kuishi kama mseja ni lazima ufanywe kati ya mtu binafsi na Bwana, kwa kuwa ni Bwana peke yake awezaye kutoa uwezo unaotakikana katika utoshelezaji ambao unapatikana kwa Mungu peke yake. Paulo anafafanua useja kama kipawa (**7**).'

'Kile Mungu Alichounganisha Pamoja…..'

Sura hii ya ndoa inazoa maswali magumu sana, na la msingi ni, 'ndoa ni nini machoni pa Mungu?' Au kwa maelezo mengine, swali hili linabibiwa katika **Mathayo 19:6:** *'…Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.'* Wakati waumini wawili wanapounganishwa katika ndoa takatifu, huwa wamesalimisha maisha yao kwa mwingine kwa kuwa wanaamini Mungu amewaunganisha pamoja. Ule ushawishi kwamba Mungu amewaunganisha pamoja ndio msingi ambao huipatia ndoa yao udhabiti, wala sio cheti kinachosema kwamba hao wawili wameunganishwa pamoja kulingana na sheria. Ikifahamika jinsi upo utofauti mkuu wa utangamano ulimwenguni katika ndoa, uamuzi wa kufanya ndoa unahitaji kuwa juu ya msingi wa uongozi wa Kiungu.

SURA YA TANO
Kanuni Tatu Za Kuishi Kama Kristo
(Sura Ya Nane, Tisa Na Kumi)

Katika maisha ya Ukristo, kuna mambo ambayo yanahesabiwa kuwa sio sawa wala mabaya lakini huambatana na hisia iliyo kinyume, kulingana na hali ya kijamii inayopatikana katika desturi au mila fulani. Katika desturi fulani, mambo haya yanaweza kuwa kama ule mfano wa kunywa divai au kutuza nywele. Katika desturi na mila za huko Korintho, ilikuwa ni katika kula chakula kilichokuwa kimetolewa kama dhabihu kwa miungu. Nje ya Kanisa, wale raia wa Korintho waliabudu miungu na kufanya matendo pamoja na kutoa dhabihu kwa niaba yao, pamoja na kutoa wanyama dhabihu ambao baadaye, nyama yao ilipelekwa sokoni kwa bei nafuu. Wengi wao katika Ukristo wangehusika katika desturi hii hapo mwanzoni kabla ya kuijia imani katika Kristo. Baada yao kuijia imani, wao waling'ang'nia kufahamu ikiwa kula chakula kilichotolewa dhabihu

kwa miungu ni vyema au vibaya, na wengi wao walihisi kuwa ilikuwa vibaya kwa kuwa kilihusishwa na bada ya miungu.

Wengine Kanisani, hasa wale waliowa na elimu au waliokuwa Wakristo kwa muda mrefu, hawakuona kosa lo lote kula chakula kilichotolewa dhabihu kwa miungu. Katika macho yao, miungu hao hawakuwa cho chote zaidi ya dhahabu, fedha au miti au mawe, na haikuwa na umuhimu wo wote wa kiroho. Hali hii ya mawazo ilitambulikana na kuhimizwa na Paulo wakati aliposema, '*…twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu il mmoja tu* (**8:4**).' Paulo hakuwa na thamani ye yote katika dhahabu na fedha, hivyo basi aliungana na wale ndugu waliokomaa kuamua kuwa kula chakula kilichotolewa dhabihu kwa miungu hakukuwa kinyume cha imani ya mtu.

'*Hata hivyo*,' Paulo alisema, *'bali ujuzi huu haumo ndani ya watu wote (***7**).' Kwa maelezo mengine, Paulo alikuwa akisema kila mtu si mwerevu jinsi wewe ulivyo. Paulo aliandika sura hizi tatu ili kujadili kile mtu aliye na maarifa kuhusu ubatili wa miungu au sanamu hizi ulivyo anachostahili kufanya wakati anapokumbana na ndugu ambaye hana maarifa hayo. Paulo anamalizia hoja hiii kuanzia anayekula chakula kilichotolewa dhabihu kwa miungu hadi katika uhusiano kati ya ndugu katika Kristo na jinsi walio na nguvu wanavyohitajika kutazamia walio dhaifu katika imani. Kwa kujibu swali hilo, wanastahili kuwa na uhuru wa kula chakula cho chote ambacho Roho Mtakatifu amewapa uhuru wa kula. Paulo aliwaambia waumini wenye uwezo, *'Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! Dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa ni dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu?* (**9,10**).'

Paulo alifahamu kuwa suluhisho hili lingewafedhehesha Wakristo 'wenye nguvu.' Alikuwa shujaa wa uhuru wa kiroho, naye alichukia mfumo wo wote wa kisheria. Hakutaka watu kubadilisha mafunzo yake na kuwa ni kitabu cha mwongozo wa yale ya kutendwa na yale ya kutotendwa katika maisha ya Kikristo. Alifahamu miongoni mwa Wakristo wenye uwezo kuwa wangechukulia suluhisho hili kwa kusema, 'kwa sababu gani uhuru wangu wa kiroho udunishwe na udhaifu wa ndugu yangu?' Paulo aliandika sura hizi ili kuwafunza Wakorintho (wewe na mimi), umuhimu kwetu kama waumini kutilia maanani mahitaji ya

ndugu zetu wadhaifu tunapofanya uamuzi wa uhuru wa kutenda kuhusu kile tunaweza kukitaja kama kuwepo katika eneo la ‘kijivu-jivu’ katika kuishi kama Kristo.

Ufupisho Wa Kanuni Tatu Za Uhuru Wa Kristo

Tunapata mafunzo ya Paulo katika sehemu hii yakiwa yamefupishwa katika maneno haya yake ya mwisho: ‘*Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu. Vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa* (**10:31-33**).’ Kutokana na mistari hii, tunachambua kanuni tatu. Kwanza, tunajifunza kwamba thamani zetu muhimu ni lazima ziwe na utukufu wa Mungu. Pili, matendo yetu yahitajika kuegemea juu ya matokeo ya wokovu wa watu wengine. Na tatu, faida ya watu wengine ni muhimu mno kuliko faida yetu wenyewe. Jambo sio lile lilo jema au mbaya, au haki yetu kutenda au kutotenda. Jambo ni lile ambalo linamtukuza Mungu, na linaloongoza hadi katika wokovu wa watu wengine, na kile kinachofaidi wengine. Unapotafakari kanuni hizi tatu, unatambua kwamba hili ni dhihirisho ambalo Paulo alinena katika waraka huu kwa njia hii: U-P-E-N-D-O-Upendo wa Mungu usio na masharti.

Ulimwengu haukubaliani na wazo kama hilo. Thamani za desturi na mila za ulimwengu huu zinadhihirishwa kupitia usemi huu: ‘sheria ya kwanza ya ustaarabu ni kujitunza mwenyewe.’ Watu wa ulimwengu huu huyaegemeza matendo yao juu ya kitu ikiwa kitakuwa na matokeo mema au mabaya kwao. Wao huuliza, ‘nitakipata nini kutokana na jambo hili?’ Lakini filosofia ya Kristo, inayofunzwa hapa na Paulo ni kuhusu kutoa – kumtolea Mungu ili upate utukufu, na kuwatolea wengine ili nao wapate kuokolewa na kufaidika.

Wokovu wetu umetufanya kuwa watumwa wa Kristo. Hatuko huru tena kutenda yale ambayo tunachagua kutenda. Tunaidhinishwa kutenda jinsi Kristo angelitenda, kutokana na kuhusika kwake kwa ajili ya wokovu na kufaidika kwa wengine kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Matumizi Ya Kanuni Tatu Za Kuishi Kama Kristo

Katika sura ya 9, Paulo alionyesha jinsi alivyotekeleza kanuni hizi tatu katika maisha yake mwenyewe. Kwanza kabisa, alitetea uhuru wake hivi: *'Je! Mimi si huru? Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu? Ninyi si kazi yangu katika Bwana? Je! Hatuna uwezo wa kula na kunywa? Hatuna uwezo kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa?'…. 'Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini? Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo* (**1, 4-5, 11-12**).' Mahali hapa, Paulo alionyesha haki yake ya kula na kunywa, na kuwa na mke kwa ajili yake mwenyewe pamoja na kukusanya mali kutokana na huduma ambayo aliitenda kwa watu wengine.

Mambo Yote Kwa Watu Wote

Kama mtume chini ya sheria ya uhuru, Paulo alikuwa huru kutenda kwa njia ile aliyoona kuwa haina upinzani kwa mafunzo ya Kristo, lakini akachagua kutoitenda. Badala yake, aliwaambia Wakorintho, *'Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo. Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja. Wala siyaandiki hayo iliiwe hivyo kwangu mimi; maana ni heri nife kuliko mtu awaye yote abatilishe huku kujisifu kwangu (***12, 15**).' Ingawa alikuwa na uhuru wa kutenda jinsi apendavyo, alichagua kutotenda hivyo kwa woga kwamba kungekuwa na kizuizi cha Injili aliyokuwa akihubiri. Kwa njia hii, aliweka utukufu wa Mungu pamoja na wokovu wa watu juu ya tamaa yake mwenyewe.

Sehemu kuu ya ujumbe wa Paulo imo katika kifungu hiki: *'Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nilijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria,) ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wali wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali*

*zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine (**19-23**).'*

Ingawa Paulo alikuwa huru kutoka kwa wanadamu, kumaanisha kuwa alikuwa mzaliwa huru wala hakufanyika kuwa mtumwa wa mtu ye yote, aliamua kufanyika mtumwa kwa watu wote kwa ajili ya Injili. Aliamua kuwatumikia kwa njia ye yote ili apate fursa kuieleza Injili ya wokovu kwao. Ikiwa mtu angekuwa Myahudi, Paulo angekaribisha matendo yake ili kuifanya Injili kuwa dhahiri na yenye kumvutia Myahudi. Na ikiwa yule mtu alikuwa hana elimu, Paulo angezungumza naye hivi kwamba Injili ingalikuwa dhahiri kwake.

Ingawa kulikuwepo na viwango ambavyo hangefikia. Kwa mfano, mtu alikuwa bila sheria, angetenda cho chote ambacho kingewezekana kuifanya Injili kuwa wazi na yenye kumvutia. Ingawa Paulo hangevunja imani yake kama wengine wangekataa, alikuwa tayari kutumia uhuru wake katika Kristo kuifanya Injili kueleweka kwa watu wote wa tabaka mbali mbali.

Paulo aliufanya uhuru kuwa mmoja wa matakwa yake makuu na kupinga mfumo wo wote wa kisheria, lakini alikuwa mwenye kuhusika sana kwa wale ndugu waliokuwa wadhaifu na wanyonge pamoja na ushirika wa mwili wa Kristo. Kuambatana na matakwa haya ya Paulo, alichagua kujitenga na desturi zo zote ambazo zingeweza kumfanya yule ndugu mnyonge kukwazwa.

Kwa matumizi, ingawa sisi tu huru katika Kristo kutenda mambo mengi, tumewajibika katika matendo yetu jinsi yanavyowahusu wengine, hasa wale ambao ni washiriki katika mwili wetu wa kiroho. Hivyo basi, ikiwa tutafanya jambo ambalo halitaenda kinyume na utakatifu wa Mungu au uhusiano wetu na Kristo, ila twakwaza ndugu, hatustahili kutenda jambo hilo machoni pao. Kanuni ambayo Paulo anafundisha haitekelezwi kwa kumfukuza yule ndugu mchanga mbali, au kwa kumwambia atatazame upande mwingine. Matumizi ya kanuni hii yanapatikana katika kuwajali kwetu pamoja na upendo wetu kwa ndugu katika Kristo, pamoja na ushirika katika mwili.

Kufahamu Wajibu Wa Mwanamke Kanisani

Katika sura ya kumi na moja ya **1 Wakorintho**, Paulo anazungumzia wajibu wa wanawake pamoja na Meza ya Bwana. Aliwafunza wanawake kufunika vichwa vyao na kukuza nywele ndefu. Paulo aliandika hivi: *'Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake. Kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala ya mavazi* ***(*****15).'** Katika desturi ya Wakorintho, wanawake wenye nywele fupi walifahamika kuwa makahaba na wenye tabia ya kutilia shaka. Hivyo basi, ili kumtenga mwanamke Mkristo, Paulo aliwaagiza kujifunika vichwa na kukuza nywele ndefu.

Haya yalikuwa mafunzo ambayo misingi yake ni desturi ya wakati ule, lakini kanuni yake ya kutengwa katika desturi ilikuwepo. Ikiwa desturi ile ambayo tunaishi kati yake huwatambua baadhi ya watu na aina fulani ya mavazi au aina ya mtindo wa nywele, basi tunastahili kutojivika aina ya mavazi yale au kukuza nywele kwa mtindo huo. Hatuhitajiki kutilia shaka lo lote ndugu hao kwa ajili ya aina ya mtindo wa mavazi yetu. Pia hatustahili kuwa na sababu ye yote kwa watu wa nje katika kuwafananisha wanawake wanaomfaa Yesu kuwa makahaba. Ikiwa desturi haiambatanishi nywele fupi na ukahaba, basi hatuna sababu ye yote kwa wanawake wanaomfuata Yesu kujivika mtindo huo wa nywele fupi.

Jinsi nilivyotambua katika ukaguzi wangu wa waraka huu, mafunzo ya Paulo kwamba mwanamke anastahili kujifunika anapoomba au anapotabiri, hayamaanishi kwamba wanawake wanahitajika kuvalia kofia wakiwa Kanisani. Hili lilikuwa likuhusiana na desturi, ambazo hata sasa ziko katika desturi za watu wa huko Mashariki ya Kati, kwamba wanawake wawe wamejifunikia kwa kujisitiri wanapokuwa katika umati wa watu. Funzo hili muhimu la Paulo linaonyesha, kwamba ingawa tunafunzwa katika waraka wa Paulo kwa Warumi kwamba hatustahili kufananishwa na ulimwengu huu **(Warumi 12:2),** hatustahili kujali mambo katika desturi zetu. Wakati wamishionari wa kike wanapoishi katika desturi za watu wa Mashariki ya Kati siku hizi, wao hufunzwa jinsi ya kujimudu katika mambo na desturi zilizopo katika eneo hilo.

Kweli kwamba Paulo anafahamu kuwa wanawake huomba na kutoa unabii wakati Kanisa linapokutana, ni hoja kwamba wajibu wa wanawake katika ibada Kanisani ni pamoja na kuomba na kuhubiri. Ukaguzi zaidi kuhusu wajibu wa wanawake katika Kanisa

unaweza kutufikisha katika uamuzi huu: Mwanamke anaweza kutenda cho chote Kanisani ikiwa tu kile anachotenda kiko chini ya usimamizi wa wazee wa Kanisa hilo. Pamoja na ukaguzi huo, kila mtu Kanisani yupo chini ya mamlaka ya wazee, nao wazee wako chini ya mamlaka ya Kristo aliyefufuka pamoja na Neno la Mungu.

Jinsi Meza Ya Bwana Inavyostahili Kuwa

Wakati Paulo alipotoa masahihisho yake kwa matumizi mabaya ya Wakorintho wakati walipokuwa wakikutana kwenye Meza ya Bwana, aliwafunza waumini hao wa Korintho kuwajali wengine na kutafakari mioyoni kabla ya kukutana kwenye meza. Alikuwa amesikia kwamba walikuwa wakishiriki katika Meza ya Bwana kwa njia isiyostahili kwa sababu mbili: Hawakuwafikiria ndugu zao katika Kristo na hawapokea Meza ya Bwana kwa njia inayostahili: ‘Kwa maana kila mmoja hutangulia kutwaa chakula chake katika kule kula; hata huyu ana njaa, na huyu amelewa **(21**).’

Ilikuwa ni desturi katika kizazi cha kwanza cha Kanisa kushiriki katika ‘Karamu ya Upendo,’ kabla ya kusheherekea ushirika mtakatifu. Kutokana na kile Paulo anachoandika mahali hapa, yaonekana kwamba wao hawakuweka chakula walichokuja nacho kwenye meza ya washirika. Yaonekana kwamba, kila mmoja wao alibeba chakula alichokuwa chake. Miongoni mwao walikuwepo matajiri hivyo basi walibeba chakula chao wenyewe, ilhali waliokuwa maskini (yamkini labda watumwa), na wao hawangeliweza kuleta chakula chao. Wale waliokuwa na chakula kingi walikula machoni pa waliokuwa hawana. Muumini mmoja alikuwa akila chakula kitamu mbele ya waumini waliokuwa na njaa. Wengine wamdhania Paulo ‘kuzimwagia maji’ karamu za maakuli Manisani wakati anapouliza*: ‘Je! Hamna nyumba za kulia na kunywea? Au mnalidharau kanisa la Mungu, na kuwatayaharisha hao wasio na kitu? Niwaambieni? Niwasifu? La! Siwasifu kwa ajili ya hayo* (**22**).’

Wao walikuwa wakishiriki katika Meza ya Bwana bila kuwajali waumini wenzio. Tunaona kwamba baadhi ya ndugu walikuwa wakishiriki katika Meza yake Bwana ili kuzitosheleza tamaa zao kwa kile kinywaji. Kwa hakika, walitumia divai ili kulewa. Tunashangaa kusoma mambo haya yasiyostahili, kwa kuwa tunalinganisha desturi na mila zetu na zile za ‘Kanisa la kwanza la Korintho.’ Ni lazima tukumbuke kwamba hawa walikuwa baadhi ya washiriki wa kwanza wa Kanisa la kwanza katika mji huo uliokuwa

umelowa kwa zinaa wa Korintho. Wale miongoni mwetu ni wazazi wa kimwili na kiroho, tunatambua kwamba watoto hujichafua kwa kinyesi chao wenyewe. Paulo anawataja Wakorintho hawa kama watoto wachanga (**1 Wakorintho 3:1**).'

Hali hii isiyokubalika ilikuwa ya kuchukiza kwa Paulo. Hali halisi ya maana ya Meza ya Bwana ni ukumbusho wa Kifo na Ufufuo wa Kristo na kile ambacho kweli hizo mbili za Injili zinamaanisha kwa waumini ambao wanakutana na Kristo pamoja na wenzio kwenye meza ile. Paulo alikemea Kanisa la Korintho kwa kuandika: '*Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe* (**27-28**).'

Katika tafsiri nyingine, kifungu hiki kinawaonya Wakorintho wasishiriki katika Meza ya Bwana kwa njia ambayo haistahili. Hii ni tafsiri isiyo na maana sanifu kwa kuwa inamfanya muumini kujihisi kuwa ni lazima wanastahili kwa Meza ya Bwana. Wakati anapotenda dhambi, wao hujitenga mbali na Meza hasa wakati ambao kwa hakika wanahiitaji. Tafsiri iliyo bora inamfasiri Paulo vyema. Alikuwa akiwapa Wakorintho (wewe na mimi), mwongozo kwamba tunahitaji kushiriki katika Meza kwa njia inayostahili. Meza hii inazungumzia kutostahili kwetu na kustahili kwake Mwokozi wetu aliyeteswa na kufufuka.

Kwa neno moja, Paulo alikuwa akiwaambia kuifanya Meza ya Bwana kuwa wakati wa kutafakari mioyoni mwao mbele za Bwana, wala sio wakati wanapokula chakula kinachovutia, ilhali waumini wenzio walio na njaa wanatazama, kisha wanafanyika walevi kwa mvinyo uliopo kwenye Meza ya Bwana.

Paulo anaonyesha kwamba ulikuwa wakati wao wa kuwa na ushirikia mmoja kwa mwingine, anapowaambia: '*Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojane* (**33**).' Umoja wa waumini pia jambo la muhimu katika Ushirika wa Meza. Kuwangojea waumini wanyonge ili mwili wote upate kushiriki pamoja katika Meza hiyo ni ishara ya umoja wetu mbele za Kristo anayeishi, ambaye kifo na ufufuo Wake tunausherehekea kibinafsi na kama kundi.

Je! Wewe unashiriki kwa njia gani katika Meza ya Bwana? Je! Wewe unakuwa na fursa ya kujichunguza kabla ya kula mkate na kunywa divai ambayo inawakilisha mwili pamoja na damu Yake iliyomwagika kwa ajili yako? Je! Unautambua umuhimu wa mwili na damu ya Kristo wakati wa ushirika wako na Mungu na kwa watu wengine katika Kristo pamoja na jamii yako ya kiroho?

Tafakari juu ya kifungu hiki chenye heshima kuu kasha ufanye wakati wako kwenye Meza ya Bwana kuwa ujuzi mtakatifu, kwako kibinafsi na katika ushirika huku ukiitimiza maana ya Meza ya Bwana katika hali ya heshima kuu na ukumbusho wa dhabihu na ufufuo Wake.

Sehemu Ya Ujenzi Katika Waraka Huu

SURA YA SITA

Kazi Ya Roho Mtakatifu

Paulo alianza sehemu hii ya ujenzi katika waraka wake wa kwanza kwa Wakorintho kwa kutangaza: *'Basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu* (**12:1**).' Waumini wa Korintho walikuwa watu waliotakaswa na wa kiroho. Walikuwa wametengwa ili kumfuata Kristo. Lakini pia walikuwa watu wa asili ya mwili. Walikuwa wametakaswa na kuitwa kuwa watakatifu, ilhali maisha yao hayakuwa na ushuhuda wa Kristo kwa kuwa walikuwa watakatifu, wasiokuwa na ufahamu. Mzigo mkuu wa mwalimu mkuu katika kizazi cha kwanza cha Kanisa baada ya Pentekoste ulikuwa ni: '*sitaki mkose kufahamu **12:1.'***

Katika kiwango cha ulimwengu, waumini wa Korintho walikuwa watu wenye elimu ya juu. Waliheshimu sana elimu, na yamkini wengi wao walikuwa na elimu kuu ya kilimwengu. Pia, walikuwa na elimu kuhusu Mungu na Roho Mtakatifu. Lakini hawakufahamu kazi ya Roho Mtakatifu. Paulo alikuwa na hamu ya kuondolea kutofahamu huko katika sehemu ya pili ya waraka wake. Alianza kwa kufundisha Kanisa hili kuhusu watakatifu walioukuwa bila ufahamu kuhusu njia ambayo Roho Mtakatifu alikuwa akitaka kuifanya kazi katika Kanisa.

Msimamo Mbaya Kuhusu Roho Mtakatifu

Kanisa la Korintho ni Kanisa ambalo tunaweza kulitaja kama ‘la Kipentekoste,’ kuwa Paulo anaanza sehemu hii ya waraka wake ambao atakuwa na mengi ya kuzungumzia kuhusu Roho Mtakatifu, kwa kutaja njia kadhaa ambazo watu hawastahili kufahamu wajibu au kazi ya Roho Mtakatifu kupitia. Atawaambia kwamba ni vibaya kutofahamu kazi za Roho Mtakatifu. Pia atawaeleza kuwa ni vibaya kujaribu kuchukulia kuwa maalumu baadhi ya kazi za Roho Mtakatifu au kuwekelea juu kazi za Roho Mtakatifu ambazo hazipo.

Roho Mtakatifu Hupeana Karama

Paulo alianza kwa kufunza kwamba Roho Mtakatifu huwapa waumini karama za kiroho: *‘Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule… Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye* **4, 8-11**).’

Wakati Roho Mtakatifu anapothibitisha uwepo wake kwa muumini, huja pamoja na karama tofauti. Huthibiti vipawa au karama tofauti kwa waumini tofauti ili waweze kuzitumia katika huduma za kipekee. Ingawa vipawa hivi ni vingi mno, navyo huwawezesha waumini tofauti kuwa na huduma tofauti, huwa vinatolewa kwao na yule Mmoja tu, Roho Mtakatifu. Vipawa hivi vya Roho Mtakatifu humfikia na kwenda kwa ajili ya Kristo aliyefufuka. Waumini wenye vipawa huhudumu kwa wengine katika Kanisa lao. Wakati hili linapotendeka, Kanisa lote hujengwa na kukamilishwa kwa ajili ya kazi ya huduma, ambayo zaidi ya kuwafikia na kuwabariki waumini; pia huenda nje katika utiifu wa Agizo Kuu.

Vipawa Vya Kiroho Hudhihirisha Utofauti

Katika sura hii, twajifunza mambo mawili yaliyo kinyume lakini yana kanuni zinazoambatana. Kwanza, tunajifunza Utofauti wa waumini wenye vipawa kwa kuwa wao wana vifurushi tofauti vya kiroho. Ikiwa wawili miongoni mwetu wanafanana kikamilifu, hakika mmoja wetu hastahili kuwepo. Watakatifu wote wenye vipawa katika Kanisani

wanahitajika. Washiriki wote hawana kipawa kimoja – baadhi yao ni waalimu, wengine ni manabii, ilhali wengine ni wenye kupambanua, wengine wana vipawa vya usimamizi na huku wengine wakiwa na vipawa vya uponyaji.

Kanisa lililojawa na Roho Mtakatifu litakuwa na watu wa aina mbali mbali, walio na vipawa tofauti vya kiroho ambavyo viko chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu sio kitu kama maji. Roho Mtakatifu ni Mtu. Aidha tuna utu wa Roho Mtakatifu au hatuna. Dhana hii ya kujawa na Roho Mtakatifu, inamaanisha kutawaliwa Naye.

Vipawa Vya Kiroho Hutenda Kazi Kama Mwili

La pili, tunajifunza kuwa kitu kimoja, au Umoja wa watakatifu katika ushirika wa Kanisani. Hii inamaanisha washirika wote wameungana katika mtu mmoja, naye ni Kristo. Hii pia inamaanisha, hata kama wapo watu tofauti wenye vipawa tofauti, wao hutenda kazi moja kwa ajili ya kusudi moja. Je! Yawezekana vipi kanuni hizi mbili zilizo kinyume kutenda kazi katika kundi moja la watu? Paulo anawasilisha kanuni hizi mbili zisizolingana pamoja na ufunuo wake kwamba Kanisa hutenda kazi kama mwili wa binadamu.

'Kwa maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo (**12**).' Miili yetu ina mikono, miguu, masikio, mapafu, na viungo vingine – tofauti – lakini kila kiungo kinatenda kazi yake kwa ushirikiano wa kuvutia sana katika mwili. Viungu hivi hutenda kazi zao tofauti ilhali vinafanya kwa ajili ya mwili wote. Hivi ndivyo mwili wa Kristo ulivyo, ambapo kila mshiriki ana kipawa tofauti, bali anaungana na mwili mwingine wote kupitia Kristo, ambaye ndiye Kichwa chetu **(Wakolosai 1:18**).

Vipawa Vya Kiroho Vyakaidi Umoja

Ni bahati mbaya, sio Makanisa yote yanayokumbatia utofauti wa vipawa vya Roho Mtakatifu. Wao hutaka washiriki wao kudhihirisha kipawa cha aina moja tu, iwe ni kipawa cha uponyaji, unabii, ndimi au cho chote. Mkazo ni kwamba vipawa vingine vya Roho Mtakatifu ni bora kuliko vingine na kuwa washiriki wao wote ni lazima wawe na vipawa hivi kama vyeti au thibitisho la Roho. Kwa maoni yangu, hili sio lile Paulo alilokuwa akifunza katika sura hizi za ujenzi za waraka huo.

Paulo aliandika: ‘Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yule yule (**4**).’ Paulo alifunza kwamba aina hii ya mwili wa kanisa haiwezi kutenda kazi vyema, huku akitumia mfano wa mwili wa binadamu ili kudhihirisha lengo hili. *‘Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa?. . . Na jicho haliwezi kuuambia mkono, Sina haja ya ninyi (***17, 21a**).’ Huo si ulinganifu. Ni kuwa na umoja. Umoja sio njia moja ambayo Mtume Paulo aliaelezea Kanisa ili kutenda kazi na Kristo.

Kanisa Lina Wajibu

Sura hii inaonyesha maana au asili na wajibu wa Kanisa. Tunajifunza kwamba Kanisa limeunganishwa pamoja kupitia umoja huo, jinsi inavyoonyeshwa kupitia mafunzo ya Paulo kuwa tu mwili ambao huongozwa na kichwa kimoja ambacho ni Kristo. Pia twajifunza kwamba washiriki wa mwili huu wana utofauti kupitia karama tofauti walizopewa kutoka kwa Roho Mtakatifu. Tunahitaji kuishi katika hali ya umoja bila kupoteza utofauti wetu. Hamaanishi utofauti wa elimu ya kithiolojia au kitaalamu. Paulo anafunza kwamba kuna hali ambayo tunaweza kusheherekea utofauti wa washiriki tofauti Makanisani mwetu bila kujeruhi umoja huo wa ajabu wa Kanisa.

Kanisa pia hutenda kazi kwa wingi wa utofauti; kumaanisha kuwa Roho Mtakatifu huwatumia washiriki <u>wote</u> Kanisani ili kutimiza kazi ya Kristo na kutangaza Neno la Kristo kwa ulimwengu. Kazi yake sio kwamba ifanywe kupitia mikono ya binadamu au wachungaji wawili, bali kupitia washiriki wote kwa njia ya karama zao.

Washiriki huko Kanisani hudhihirisha huruma yao kwa wenzao jinsi Paulo anavyosema: '*Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza?* (**29**).' Hatimaye, washiriki wa mwili wa Kristo hutenda kazi kwa usawa. Ingawa vipawa vyetu ni tofauti, hivyo pamoja na waumini vinadhihirishwa kupitia wao. Wana thamani moja machoni pa Mungu. Kwa sababu hii, kiongozi mkuu wa Kanisa la Agano Jipya, Yakobo, alitaja tatizo hili la kuwabagua watu kuwa ni dhambi (**Yakobo 2:9**). Ingawa baadhi ya waumini wenye vipawa pamoja na huduma hawatambulikani sana, wangali na thamani kwa Kristo mwenye Kanisa. Mungu aliunganisha mwili kwa njia hii '*Ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vyote hufurahi pamoja nacho* (**25**).'

Vipawa Ni Vya Maongozi

Wakorintho wa kwanza sura ya **14** inaonyesha kile kinachotendeka wakati Kanisa linapokuza kipawa kimoja juu ya kingine, hasa kipawa cha ndimi. Miongoni mwa Kanisa la Korintho, wale walionena kwa ndimi walijitambua kuwa bora kuliko wale ambao hawakunena. Walikuza ndimi kama vyeti vyao vya ujuzi wa kikristo, badala ya wajibu unaotarajiwa kutoka kwavyo kama mojawapo ya vipawa vya Roho Mtakatifu alivyowajalia waumini kumiliki. Swali bora linastahili kuwa kuhusu dhihirisho la kipawa hiki cha Roho Mtakatifu: Je! Kunena kwa ndimi ndio ujuzi wa Ukristo, au ni ujuzi wa baadhi ya Wakristo?

Shida Tatu Za Kanisa Lenye Vipawa

Wakati vipawa vya Roho vinapofanya kazi Kanisani, huwa vinatabua shida. Ni heri kwa wachungaji wengi kuwa na shida ambayo huambatana na vipawa hivyo kuliko kuwa na nidhamu bila uhai wa kiroho utokanao na vipawa hivyo huko Kanisani. (Maiti ina nidhamu, lakini iko katika hali ya ufu). Shida hizi huanza na ubaguzi. Wale ambao wanao uwezo hudhania kuwa wana vipawa au uwezo bora, huku wakiwabagua wale ambao hawana vipawa vya aina hiyo. Ubaguzi huu huleta kudunisha kwa wale ambao hawana namna ya vipawa vya kiroho au wenye mfumo wa huduma ile. Kwa kuwa baadhi ya waumini huwa hawana usalama wa kiroho, washiriki hao ambao wanadunishwa huanza kujitilia shaka kiroho. Washiriki hawa waliodunishwa mara kwa mara hutoroka Kanisa, huku shida la tatu ambalo ni mgawanyiko likiibuka.

Mwishowe, mgawanyiko huu unaweza kukua hadi kiwango ambacho washiriki huvunjika-vunjika miongoni mwao na kuunda makundi tofauti ambayo huwapa uhuru wanaotaka. Kuna vivuli na viwango mbali mbali elfu mbili vya aina ya Kiprotestante vya mwili wae Kristo. Ikiwa mwili wako ungengawanyw'a katika viungu elfu mbili, je! unaweza kuhudumu vyema? Shida hizi tatu yaani, Ubaguzi, Kudunisha na Mgawanyiko zimehatarisha na kuharibu mwili wa Kristo kote ulimwenguni.

Ili kufanya tatizo hilo lisikweze kwa kiwango hiki, Paulo aliwakabili Wakorintho. Aliwaambia wale waliokuwa wakikweza kipawa cha ndimi dhifdi ya vipawa vingine jinsi kuwa kipawa hiki si cheti au kitambulisho. Miongoni mwa vipawa vilivyoorodheshwa katika sura ya **12,** kipawa cha ndimi ndicho cha mwisho ambacho kinaweza kutumika kama cheti, kwa kuwa vipawa vyote vya Roho hupeanwa ili kuwajenga washiriki wengine. Kipawa cha ndimi kisipotumiwa pamoja na mkalimani, hakitendi cho chote katika kujenga mwili wa Kristo: '*Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga Kanisa (**1 Wakorintho 14:4**).'*

Paulo alitofautisha kipawa cha ndimi pamoja na cha unabii ili kuonyesha wale waliokuwa wakikweza kuwa hawakifahamu vyema. Hawakufahamu kwamba kipawa chao kinastahili kutumiwa katika ujenzi wa mwili wa waumini. Kwa hakika, walikuwa na kiburi kwa 'lugha maalumu ya maombi' ya wanaoshiriki na Roho Mtakatifu, ambayo washiriki wengine Kanisani hawakuifurahia. Ingawa lugha ni safi na imetolewa na Roho Mtakatifu, hatimaye inahitajika kutumiwa ili kujenga mwili wa Kristo kutumia mshiriki mwingine ana kipawa cha ukalimani (**1 Wakorintho 14:27,28).**

Paulo aliwahimiza Wakorintho kutumia vipawa vyao tofauti kwa ajili ya faida ya mwili wote*: 'Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, Kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga* **(26).'** Kwa maelezo mengine, vipawa vyetu vya kiroho vyahitajika kutumiwa kwa ajili ya kujenga mwili wa Kristo. Vimetolewa ili kuukuza umoja wetu na kutia nguvu vipawa vyetu pamoja na huduma.

Matumizi

Mtindo wa huduma/kipawa chako ni upi? Je! Umevumbua jinsi Roho Mtakatifu anavyokupa wewe, na kukuwezesha pamoja na kukuhimiza kutumia kipawa alichokupa?

Je! Unawezaje kutumikia vyema mwili wa Kristo kupitia kipawa chako? Kiwe kipawa chako ni cha kufundisha, kutambua, hekima, uinjilisti, usimamizi, usaidizi, rehema, uponyaji au kingine kile Paulo alichoelezea. Roho Mtakatifu amekutayarisha kwa uwezo unaohitaji ili kumtukuza na kulijenga Kanisa Lake. Kagua orodha zilizopo katika Maandiko kuhusu zaidi ya vipawa ishirini na kwa njia ya maombi, tilia maanani orodha hiyo hadi wakati Roho Mtakatifu pamoja na washiriki wengine kanisani watakapo kusaidia kuvumbua kipawa chako. Kulingana na Paulo, hakuna mshiriki asiye na kipawa katika mwili wa Kristo. Anza kutumia vipawa vyako leo, kisha uone jinsi Bwana atakavyozidisha juhudi yako kwa ajili ya utukufu Wake.

SURA YA SABA

Upendo Ni Nini?

(Sura Ya Kumi Na Tatu)

Paulo alizungumzia mambo mengi katika waraka wake wa kwanza kwa Wakorintho na kupeana jibu kwa kila moja ya shida. Lakini aliwapa suluhisho moja ambalo linaweza kutumika katika kila tatizo la kiroho ambalo Wakorintho walikabiliana nalo na kila tatizo ambalo tutakakumba nalo Makanisani mwetu. Suluhisho hili ni Upendo.

Kitu Kikuu Ulimwenguni

Sura kuu ya upendo kwa hakika, inaanza katika msitari wa mwisho wa sura ya **12**: *'Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora* (**12:31**).' Katika sura ya **12**, Paulo alikuwa akijadilia kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu ambayo ni kuwapa waumini vipawa. Katika sura ya **13,** Paulo alionyesha kwamba upendo ni kitu kikuu ulimwenguni: *'Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu* (**13:1-3**).'

Paulo alianza sura kuu ya upendo kwa kulinganisha dhamana ya upendo kwa kile kilichokuwa kimedhaminiwa mno na Wakorintho. Kwa kuwa waliudhamini usemi wenye usanifu na walichukulia kipawa cha kunena kwa lugha kuwa ndio cheti, alisema kwamba

ikiwa nitanena kwa lugha za wanadamu (usemi wenye usanifu mkuu) na za malaika (kuzungumza kwa ndimi), na sina upendo, mimi ni sawa na kelele nyingi sana.

Hawa Wayunani wenye elimu nyingi walidhamini kuelimika, na hivyo Paulo anasema kwamba upendo ni muhimu zaidi kuliko kujua mambo yote. Kama Kanisa lake, Wakorintho walidhamini sana unabii na kuelewa mafumbo. Kwa sababu hiyo, Paulo alitangaza kwamba ikiwa nina kipawa cha unabii na kuelewa siri na mafumbo yote ulimwenguni, na sina upendo, basi ni bure

Pia alisema kwamba ikiwa nitasalimisha mali yangu na kuwalisha maskini na kuutoa mwili wangu uchomeke motoni na sina upendo, kujitolea kwangu ni bure. Hapo mwanzoni mwa waraka huu, Paulo alitambua kwamba waumini Wa-Korintho walikuwa na vipawa vingi (***1:7***). Kulingana naye, hakuna kitu tunachokosa, wala tulicho nacho kwa njia ya kipawa, na hakuna cho chote tuwezacho kutenda ambacho kinaweza kuchukuwa nafasi muhimu wa upendo maishani mwetu kwa kuwa upendo ndio kitu kikuu ulimwenguni. Ni dhahiri kwamba Paulo alikubaliana na mtume Yohana kwamba Mungu ni upendo. Hii ndio sababu upendo ndio kitu kikuu ulimwenguni na hakuna cho chote nisicho nacho au nilicho nacho, wala hakuna cho chote niwezacho kutenda ili kuchukua nafasi muhimu ya upendo maishani mwangu.

Kuna maneno kadha ya Kiyunani yanayotumiwa kwa upendo. Neno ambalo Paulo anatumia hapa ni ‘Agape.’ Maneno mengine ya Kiyunani yadhihirisha ukarimu au huba. Neno hili ndilo linalotumika kuelezea jinsi Mungu anavyo tupenda na vile tunavyoweza kuwapenda wengine wakati upendo wetu ni ule Paulo anaotaja kama tunda la Roho (**Wagalatia 5:22,23**).

Hatuwezi kuifafanua thamani ya upendo, lakini tunaweza kutoa maelezo kuhusu tabia na thamani yake. Katika msitari wa nne hadi wa saba, dhana ya upendo inapitizwa kwenye kioo cha pembe au pande tatu katika mawazo ya Paulo na kutokea upande mwingine kama furushi la tabia za wema kumi na tano: ‘*Upendo huvumilia, Upendo una wema, na hauna wivu; upendo haujivuni na wala hautakabari, hauna tabia mbovu, haujitafutii yake mwenyewe, hauakasirishwi, hauyasebu makosa, hauyafurahii mabaya, ila huufurahia ukweli; huyavumilia yote, huyaamini yote, huyatumainia yote.’*

Upendo Hauwezi Kuharibiwa

Kulingana na kifurushi hichi cha wema, kuna maoni mengi ambayo twaweza kutoa kuhusu upendo wa Agape. Kwanza, upendo hauwezi kuharibiwa. Una uvumilivu na huyavumilia yote; na hivyo kudumu kuliko mengine yale. Upendo una nguvu. Tunapompenda mtu kwa upendo wa Agape, twaweza kumwambia kwamba hakuna kile atakachosema au kutenda kitakacho tufanya kuacha kumpenda, kwani tunampenda kwa upendo wa agape wa Mungu, nao upendo wa Mungu una nguvu. Hata hivyo, hivi ndivyo Mungu anavyotupenda. Hali tukiishi maisha ya dhambi, Mungu alituonyesha upendo Wake kwa kumtuma mwanawe ili afe kwa ajili yetu (**Warumi 5:8**). Tunapowapenda watu kwa upendo wa aina hii ambao hauwezi kuharibika; ambao Mungu anatupenda, basi tutawapenda kwa upendo wenye nguvu ambao hauwezi kuharibiwa.

Upendo Usio Na Masharti

Upendo hauna masharti. Haumpendi mtu kulingana na yale asiyotenda au anayotenda. Upendo huu hautegemei matendo. Upendo wa binadamu ni kinyume. Sisi huwawekea watu masharti yanayotarajiwa ili wawe na tabia ya aina Fulani, huku tukiwapa upendo wetu wakati wanapokuwa na tabia hiyo tunayotarajia. Hivi ndivyo wazazi wengi wanavyo wapenda watoto wao' jinsi waume na wake wengi wanavyo pendana. Lakini mtu apendwaye kwa njia hii hujihisi kuwa hana usalama. Wao huwa hawana ufahamu kuwa tabia yao itakubaliwa. Wana hofu kuwa wanaweza kukosa kutimiza matarajio yao. Hata wanapotimiza matarajio yetu, huwa hawawezi kuhakikisha kwamba wanaweza kuendelea kutimiza matarajio hayo.

Lakini upendo wa Agape hauko hivyo. Hauna masharti. Tunapopendana pasipo masharti, hatuweki hesabu ya makosa tunayotendewa ili kuthibitisha kwamba mtu huyo hastahili upendo wetu. Tunapopendana bila masharti, upendo wetu hauwezi kushindwa, na watu hawawezi kuwa na hofu kuwa tungali tunawapenda. Kwa mara nyingine, hivi ndivyo Mungu atupenda. Ingawa tutaendelea kupungukiwa na utakatifu Wake, Yeye huitenganisha dhambi yetu '*mbali kama ilivyo mashariki kutoka magharibi* ***(Zaburi 103:12)****,* bila kushindwa kutusamehe na kuyasahau makosa yetu. Upendo Wake kwetu hautegemei kile tunachotenda au kile tusichotenda; na hivi ndivyo twahitajika kuwapenda wengine.

Upendo Wenye Kuhimiza

Upendo huhimiza. Hauamini mambo yote na hutarajia mambo yote, jinsi Kristo alivyo wapenda mitume. Wakati Yesu alipokutana na Petro, alimwita Kefa, maanake, '*Mwamba (**Yohana 1**:**42**).*' Ingawa maisha ya Petro yalikuwa yamejaa msuko-suko, Yesu alimwita Mwamba kwa muda wa miaka mitatu, kasha baada ya miaka hiyo alisema hivi, *'Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu mimi nitalijenga Kanisa langu; nayo milango ya kuzimu, haitalishinda* (**Mathayo 16:18,19**).'

Jaribu mpango huu wa upendo kwa watoto wako. Watoto huishi jinsi tunavyotarajia. Ikiwa tutawataja watoto wetu kuwa hawajiwezi, inawezekana kuwa wataishi kulingana na matarajio yetu. Lakini ikiwa tutawapenda kwa upendo wa 'agape', ambao huwapa tumaini, tutaona wana wetu wakifikia na kupita yale matarajio ya uweza wao mkamilifu. Ilhali tukiendelea kuwapenda wana watu kwa upendo huu bora, ambao huwapi tumaini katika utaratibu huu imani, matumaini yetu hufanyika kuwa yao. Wao hufikia mahali wanapokuwa na imani katika uwezo wao binafsi kisha huwa na tumaini ambalo wakumbana na matarajio yao. Haya ndio ninayomaanisha ninaposema kwamba upendo wa agape ni wa kuhimiza.

Upendo Haushindwi

Baada ya kutoa maelezo kuhusu jinsi upendo unavyofanana, Paulo alirudi kwenye somo hili kuhusu vipawa vya kiroho. Alionyesha kuwa vipawa vya roho haviwezi kuchukua nafasi ya upendo kwani upendo unadumu kuliko mambo mengine yale: '*Bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika* (**8b-10**).'

Wakati Yesu Kristo atakaporudi, hatutahitaji unabii. Tutakapo mwona uso kwa uso na kumfahamu, hatutahitaji ufahamu wa kibinadamu ulio na kipimo. Vipawa vyote vya kiroho siku moja vitapita, lakini kuna thamani tatu zitadumu milele: '*Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo* (**13**).'

Tumaini ni kusadiki ambako Mungu ameweka katika mioyo yetu kwamba kuna jambo jema katika maisha haya na kwamba tutakipokea. Tuna tarajia kwamba kuna kitu nje

ya ulimwengu huu chema. **Waebrania 11** huelezea tumaini hili na kuliunganisha na imani*: 'Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana* (**Waebrania 11:1**).' Hii inamaanisha kwamba tumaini ndio msingi wa kusadiki anaotupatia Mungu ili kutuongoza hadi kwa imani. Imani hujenga juu ya msingi wa tumaini na kupeleka tumaini hilo kwenye imani. Imani hutuongoza kwa Mungu. Sura ya imani pia inatuambia kuwa hatuwezi kumjia Mungu bila imani (**Waebrania 11:6**).

Hoja ambalo Pualo anajaribu kuwasilisha hapa katika msitari wa mwisho wa sura ya upendo ni kwamba, tumaini huleta imani, nayo imani hutuleta kwa Mungu, lakini tunapokumbana na upendo wa agape, hatujakutana na kitu ambacho kinatuelekeza katika uwepo wa Mungu kwa sababu, Mungu Ni upendo. Thamani hii ya upendo ndio utu halisi wa Mungu. Hivyo basi, Paulo anataja upendo kuwa kitu kikuu miongoni mwa thamani zile tatu zenye kudumu maishani na kutuambia kwamba kufuata upendo wa agape kunastahili kuwa hamu yetu kuu maishani.

SURA YA NANE
Ufufuo Wa Waumini Wote
(1 Wakorintho 15)

Sura ya 15 ndio ya ufufuo katika Biblia. Ufufuo ni moja wapo ya mambo ya kiroho ambayo Paulo aliwapa Wakorintho kama jawabu kuu kwa shida nyingi walizo nazo Kanisani. Wana filosofia wa Kiyunani walishuku matukio mengi yaliyokuwa si ya kawaida. Ingawa Wakorintho-Wayunani hawa walikuwa waumini, urithi wa desturi na mila zao uliendelea kugusa mawazo yao huku mzigo wa elimu ukiwafanya kutilia shaka matukio yasiyo ya kawaida; hasa kiyama cha Kristo na waumini wale waliokufa. Kama Wakorintho hawa hawangeshuku na kuuliza maswali kuhusu ufufuo, hatungekuwa na jibu hili kuu lisilo na kifani la Paulo juu ya kiyama cha Kristo pamoja na waumini waliokufa; ambalo liko katika sura ya kumi na tano la Wakorintho wa kwanza.

Paulo aliwakumbusha kwamba kiyama cha Yesu Kristo kilikuwa sehemu muhimu ya Injili aliyokuwa akihubiri, ambayo walikuwa wameliamini: '*Basi ndugu zangu, nawaarifu ile Injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama,*

na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri; isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko (**1-4**).'

Hii ndio Injili ambayo imewaokoa na ilikuwa msingi wa mfumo wa imani yao yote. Punde tu wakati Paulo alipotaja kiyama cha Yesu Kristo kama nusu ya ujumbe wake wa Injili, aliandika mistari **54** juu ya jambo hili kuhusu kile tunachoweza kutaja kama 'matumizi ya ufufuo.' Paulo alitangaza kwamba kiyama cha Kristo kinaweza kuthibitishwa kutokana na ushuhuda wa wengi walio shuhudia: *'Na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale thenashara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake* (**5-8**).'

Wakorintho waling'ang'ana sio tu kuamini katika ufufuo wa Kristo, bali pia katika waumini waliokufa wakati Yesu Kristo atakaporudi. (Paulo tayari alikuwa amewafunza Wakorintho kuhusu kuja kwa pili kwa Yesu Kristo). Paulo aliunganisha ufufuo au kiyama cha waumini na cha Kristo, akiutaja huo wa Kristo kama 'matunda ya kwanza' ya wale wataofufuliwa (**20**). Kama hatutafufuliwa, basi Kristo hakufufuliwa na hivyo basi imani yetu haina maana (**13-14**). Wakati Kristo alipokufa juu ya msalaba, alichukua mzigo wa dhambi zetu mwenyewe. Lakini alipofufuka katika wafu, alidhihirisha ushindi wake juu ya mauti. Kwa sababu hii, ufufuo Wake ni sehemu muhimu ya imani. Ufufuo wa miili yetu ni utekelezaji wa ufufuo au kiyama cha Yesu Kristo katika kifo na ufufuo wetu wenyewe.

Wakorintho walishangazwa ikiwa, 'tutafufuliwa katika wafu, basi itatendeka vipi na miili yetu itakuwa vipi?' Msimamo wa Wakorintho hawa wasomi ulikuwa kwamba hawakuamini katika ufufuo wa waumini kwa kuwa hawakufahamu jinsi ingelifanyika. Ili kuzungumzia mawazo haya, Paulo alilinganisha ufufuo wa wafu na kupandwa kwa mbegu: *'Ewe mpumbavu! Uipandayo haikuki, isipokufa; nayo uipandayo, huupandi mwili ule utakaokuwa, ila chembe tupu, ikiwa ni ya ngano au nyingeneyo; lakini Mungu huipa mwili kama apendavyo, na kila mbegu mwili wake* (**36-38**).'

Mbegu katika ardhi hufanyika ua lenye kuvutia, kama la nyungi nyungi au la waridi, ingawa hatuna ufahamu jinsi inavyotokea. Mbegu iliyopandwa haifanani na lile ua ambalo huchipuka kutoka ardhini. Jinsi Mungu anavyobadilisha ile mbegu na kuwa mmea, Yeye ataubadilishi mwili wetu wenye kuchakaa na kuwa hauchakai wakati wa ufufuo: *'Kadhalika na kiyama ya wafu. Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutokuharibika; hupandwa katika aibu; hufufuliwa katika fahari; hupandwa katika udhaifu; hufufuliwa katika nguvu; hupandwa mwili wa asili; hufufuliwa mwili wa roho. Ikiwa uko mwili wa asili, na wa roho pia uko* (**42-44**).'

Mungu hutupa miili ya ulimwengu ili tupate kuishi katika dunia hii, na ni lazima kwamba Mungu atatupatia miili ya mbiguni ili kuishi huko mbiguni. Miili yetu inayochakaa pamoja na damu haiwezi kuingia katika ufalme wa mbinguni, hivyo basi ni lazima Mungu aibadilishe miili yetu ya ulimwenguni ili atuandae kuishi katika hali ya uzima wa milele kwenye milki ya milele. Hili ndilo atakalotimiza kupitia ufufuo wetu. Wale watakao kuwa wangali hai wakati Kristo atakaporudi lazima pia wapate kubadilika 'kwa kufumba na kufumbua macho **(53**).' Tafsiri ya Kiyunani hapa ni, 'atomo.' Huku Paulo akitangaza mabadiliko haya, alifunza kwamba ni lazima matatizo mawili yasuluhishwe ili kututayarisha kuingia mbinguni. Sehemu yetu ambayo huchakaa (miili yetu) ni lazima ifanywe kuwa haitachakai na sehemu yenye kikomo kufanyika kuwa bila kikomo. Baada ya miujiza hii miwili kutimizwa, tutakuwa tayari kwenda mbingu. Neno 'Ufufuo' linamaanisha, 'ushindi juu ya mauti. Ufufuo wa waumini waliokufa utatatua matatizo haya mawili na utakuwa ndio ushindi wake muumini juu ya mauti. Hii ndio sababu Paulo anamalizia hoja hii kwa kutangaza kifo pamoja na ufufuo wa muumini kuwa ni ushindi! (**54-57**).

Paulo alitekeleza mafunzo yake juu ya ufufuo kwa waumini kwa kuwaambia, *'Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana (***58**).*'* Waandishi wote wa Maandiko wanatuambia kuhusu kuja kwa Yesu Kristo mara ya pili kwa kuwa tukio hilo ndio tumaini la baraka kwa Kanisa ulimwenguni.

Tambua kwamba manabii na mitume wakati wote hutaja sababu ya kutuambia kuhusu kurudi kwa Yesu na matokeo yanayoambatana na tumaini hilo kama ufufuo wetu.

Katika msitari huu wa mwisho wa sura hii ya ufufuo, Paulo aitekeleza Injili ya ufufuo ili kuwahimiza waumini kutenda kazi ya Bwana. Ni kana kwamba atatuambia kuwa tuko katika kundi linalo shinda na thamani ya uzima wa milele wetu itakusudiwa kulingana na kiwango ambacho tu sehemu ya ushindi huo.

Wakili Mwaminifu: (1 Wakorintho 16)

Waumini wengi hujihisi kufedheheshwa wakati Paulo anapowainua kwenye kilele cha mbinguni cha Injili na kweli ya ufufuo katika sura ya kumi na tano, kasha baadaye kusema, ‘kwa habari ya ile changizo.’ Twahitaji kufahamu jambo moja kuhusu changizo hili na pia tunafaa kupokea sababu ya Paulo kuweka jambo hili pahali hapa katika waraka huu.

Paulo alimalizia waraka huu wa kwanza kwa Wakorintho kwa kuwauliza kuchanga kwa ajili ya waumini wa Kiyahudi waliokuwa wakipitia katika dhiki ya mateso pamoja na janga la njaa lililowakumba. Aliiweka hoja hii ya wakili mwaminifu katika sehemu ya ujenzi ya waraka wake kwa sababu uwakili ni moja wapo ya ‘mambo ya kiroho’ ambayo alikuwa ametueleza katika mistari ya kwanza ya sura ya kumi na mbili, alipoanza sehemu ya ujenzi ya waraka huu. Pia, aliweka hoja hii hapo kwa sababu uwakili uaminifu ni moja wapo wa nidhamu za kiroho ambazo hudhihirisha afya ya kiroho na kuwa na nguvu kwa muumini.

Huu pia ni ufunuo wenye kuvutia katika kweli ya maisha ya mtume Paulo ambaye alikuwa mmoja wa viumbe anavcyotueleza katika maandiko yake (**Wakorintho 5:17; Wagalatia 6**:**15).** Neema ya Mungu, hubadilisha maisha, na ndio Injili ya Kristo. Paulo alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wakieneza hofu ndani ya maisha ya waumini huko Yerusalemu na Uyahudi (**Matendo 8:3; 9:1; 13, 14**). Sasa, anapokea mchango kutoka kwa waumini wa kimataifa ambao alikuwa amewaleta kwa Kristo ili kuwasaidia waumini wa Kiyahudi ambao hapo awali, alikuwa akiwatesa na kuwapeleka gerezani, hata kuua baadhi yao.

Waraka Wa Pili Wa Paulo Kwa Wakorintho

SURA YA TISA

`

Hati Ya Mhudumu

(2 Wakorintho 1-6)

Paulo aliandika waraka wa kwanza kwa Wakorintho akiwa Efeso, na kuutuma kwa mkono wa Tito. Tito aliuwasilisha waraka huo kwa Wakorintho na kukaa pamoja nao huku akifafanua yaliyokuwa yameandikwa na pia kutetea yaliyokuwemo dhidi ya wale waliohusika katika shida zile zilizokuwa zimejadiliwa katika waraka huo. Hata hivyo, Paulo alilazimika kuhama kutoka mji wa Efeso kwani kulizuka mgomo kwa sababu ya huduma yake (**Matendo 19**). Alisafiri hadi Troa kasha baadaye Filipi, ambako alimgonjea Tito arudi akiwa na ujumbe kutoka Korintho kuhusu jinsi walivyokuwa wamepokea waraka huo wa kwanza.

Habari nyingi zilikuwa njema. Wakorintho walikuwa wamemkaribisha Tito kwa upendo na ukarimu, na yale yote Paulo aliyokuwa amewahimiza kutenda katika waraka wa kwanza walikuwa wametii. Lakini baadhi ya habari hazikuwa njema. Baadhi ya watu katika Kanisa walikuwa wameanza kuvamia utume wa Paulo, ilhali wengine wakiikosoa usemi wake. Wengine walimdhania kuwa alikuwa amerukwa na akili, au ‘hakuwa mwenyewe (***2* Wakorintho 5: 31**).’ Zaidi ya hayo, wengi wao walikuwa wamekwazwa kwa kuwa Paulo hakuwatembelea mwenyewe. Lakini wakosaji wake hawakukataa baadhi ya mambo ambayo Paulo alizungumzia katika waraka wake kwani hoja yake haingepingwa. Badala yake, walimvamia Paulo binafsi. Naye aliposikia mambo hayo, aliwaandikia waraka huu wa pili.

Sura sita za kwanza za Wakorintho wa pili zinafafanua hati za mhudumu au mhubiri, kwani hili ndilo lililokuwa hoja kuu la wavamiaji wa Paulo. Walimchukulia kana kwamba hastahili wadhifa wa mtume, na hivyo hakuhitimu kuwakosoa. Paulo aliandika waraka huu ili kutetea utume pamoja na wajibu wake kama mhudumu wa Injili. Kwa sababu hiyo, tunazileta pamoja kanuni muhimu kuhusu hati au cheti chake mtumishi kutokana na maneno yake.

Wale ambao wana mwito katika huduma ya uchungaji leo watambulikana kama wahudumu wa Injili. Hata hivyo, wakati Paulo anapotumia neno, ‘Mhudumu’ hamaanishi mhubiri, bali huduma ambayo kila mfuasi halisi wa Kristo ana mwito wake.

Sura ya nne ya waraka wa Paulo kwa Waefeso inatufunza kwamba wale ambao wameitwa kuwa Wainjilisti, Wachungaji, pamoja na Waalimu wamepewa vipawa hivi *'kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe* (**12**).' (Wakati waumini walipotakaswa, au kutengwa ili kumfuata Kristo, Paulo aliwaita watakatifu.) Kwa maelezo mengine, masharti ya huduma yake Mchungaji/Mwalimu ni kumwezesha yule tunayemtaja kama 'mfanyi kazi wa kawaida' kutenda 'kazi ya huduma.' Kazi ya huduma haijatengwa kwa watu ambao wamehitimu tu, kama vile wachungaji, bali kwa washiriki wote Kanisani. Kuna aina ya washiriki Kanisani ambao wanahitajika kuwa wahudumu.

Kumtayarisha Mhudumu

Paulo anaeleza jinsi Mungu hututayarisha kuwa wahudumu wake. Njia moja ambayo hufanya hivi ni katika kutufunza jinsi ya kuwafariji wengine ambao wanapitia katika dhiki. Yeye hutenda hivi kwa kuturuhusu kuipitia dhiki kwanza*: 'Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehemu, Mungu wa faraja yote; atufarijie katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwana Mungu* (**1:3-4**).'

Wakati tunapopitia katika dhiki, huwa tunaongozwa kwa Mungu huku tukivumbua kwamba Yeye, Mwenyewe anaweza kuwa faraja tunalohitaji maishani mwetu nyakati za dhiki. Kwa kupokea faraja kutoka kwa Mfariji wa kweli, tunawezeshwa kuwafariji wengine walio katika dhiki. Kupitia dhiki yetu, huwa tunahitimu na kuwa wahudumu wa faraja, tukiwa mashahidi wa kweli kwa faraja tuliyopata wakati tulipokuwa katika dhiki. Mwinjilisti ni maskini mmoja akimwambia mwingine mahali mkate upo. Mhudumu wa faraja, jinsi Paulo anavyo mfafanua ni, moyo mmoja unaoteseka ukiambia mwingine pale faraja ipo.

Paulo alitaja kuhitimu kwa muhudumu ambaye Mungu anaweza kumtumia, kwa kuwaambia Wakorintho kuhusu mateso yake huko Listra, ambako alipigwa kwa mawe kwa ukatili mkuu kiasi cha kufa:

'Maana ndugu, hatupendi, msijue habari yya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu, hata tukakata tamaa ya kuishi. Naam, sisi

wenyewe tulikuwa na hukumu ya mauti katika nafsi zetu; ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu, awafufuaye wafu, aliyetuokoa sisi katika mauti kuu namna ile; tena atatuokoa; ambaye tumemtumaini kwamba atazidi kutuokoa (**8-10**).'

Kwa njia ya kusitirika, Paulo alikuwa akithibitisha ukweli wake kama mhudumu wa imani. Alifungua waraka wake kwa hoja ya jinsi mateso yake yalivyomwelekeza kwa Mungu na kutufanya kuhitimu kuwa wahudumu wa faraja. Kisha akawaonyesha jinsi alivyokuwa amehitimu na kuwa mhudumu. Huko Listra, Mungu alimruhusu Paulo kuteswa kupita kiasi cha uvumilivu – hadi alipopoteza matumaini ya ya kuishi – ili apate kujifunza jinsi ya kumtumainia Mungu bali si yeye mwenyewe. Punde tu alipojifunza kutojitegemea mwenyewe, alifahamu kwamba ni Mungu peke yake awezaye kumkomboa kutokana na yale ya kutisha. Wengine wanaamini kwamba Paulo anatuambia kuwa alipata ujuzi wa kufa na kufufuka wakati alipopigwa kwa mawe huko Listra. Ilhali wengine wanaamini kwamba alitumia usemi wa mafumbo katika mistari hii.

Wadhifa Wa Mhudumu

Je! Wadhifa wa mhudumu ni upi? Paulo alijibu swali hili: *'Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea; katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima. Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo? (***2:14-16**).'

Kulingana na Paulo, sisi kama wahudumu wa Injili tu kama maua, huku tukiota manukato yenye harufu ya kuvutia ya Kristo po pote tunapokwenda. Harufu hii ya kuvutia aidha huwavutia wengine katika wokovu pamoja na uzima wa milele au huwafukuza na kuwaelekeza kwenye mauti. Ikiwa wao wataikata ile harufu ya manukato, basi huwa wanamkataa Kristo na njia yao inaelekea kwenye mauti. Lakini wakivutiwa kwa Kristo kupitia manukato Yake ambayo ni sisi, basi watapata wokovu Wake pamoja na uzima wa milele.

Uzito wa wajibu huu ulimfanya Paulo kuuliza swali hili, *'Ni nani aliyetosheleza kwa mambo haya?* (**16**).' Sisi hatutoshelezi hata kuifanya tofauti kati ya uzima wa milele na mauti ya milele kwa watu ambao tunakutana nao katika maisha yetu ya kila siku, ila

kwamba Mungu atosha: '*Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu* (**3:5**).' Kupitia Roho Mtakatifu, maisha hubadilishwa. Sisi tu vyombo ambavyo Mungu hutumia kueneza harufu Yake ya kuvutia; harufu nzuri ya manukato kutoka kwa Kristo ambaye amebadilisha na anazidi kubadilisha maisha yetu.

Ni Kipi Kinachotia Motisha Wapeaji Motisha? (Sura 5:13-6:1,2)

Wakati Paulo alipojitetea kinyume cha mashtaka yao kwamba alikuwa amerukwa na akili, aliufunza juu ya wadhifa mwingine wa mhudumu. Kwa lugha ya Kiyunani, shitaka lile linatafsiriwa kwamba Paulo alikuwa 'mchoyo.' Walimshitaki kuwa alikuwa akitenda kazi kutoka kina tofauti na kile chao. Kwa kuwa Wakorintho hawa wakosoaji walikuwa watu wa kujipenda wenyewe, Paulo alikubaliana nao kwamba alikuwa na hatia kulingana na mashitaka yao. Alikuwa katika kina tofauti na chao. Kristo alikuwa ndiye kina chake ambacho maisha yake yalizungukia. Hivi ndivyo alivyomaanisha alipoandika: '*Maana ikiwa tumerukwa na akili zetu, ni kwa ajili ya Mungu; au ikiwa tunazo akili zetu timamu, ni kwa ajili yenu (***13**).'

Utetezi wa Paulo kuhusu 'kujitakia mwenyewe' ulikuwa kwamba upendo wa Kristo na mwito wa huduma yake ulikuwa kina cha maisha yake: '*Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu* (**14-15, 20a**).'

Mambo Matatu Ya Uhakika Kwa Paulo

Matendo ya Paulo msingi wake ulikuwa juu ya mambo matatu ya uhakika: Kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya watu wote, watu wote wamepotea, na kwamba ni lazima watu wote wasikie ujumbe wa Injili. Kristo pamoja na haya mambo matatu ya uhakika ndio kina cha motisha Yake; aliishi kama mtu mwenye kujitakia mambo yake mwenyewe (**18**).

Viwango Vya Uhusiano

Katika kifungu hiki, pamoja na dirisha katika kina kikuu cha motisha ya moyo wa Mtume Paulo, tuna maelezo kuhusu viwango vitatu vya kukomaa kiroho. Viwango hivi vinatueleza uhusiano wetu na Kristo katika njia tatu: '*Naye Kristo, Katika Kristo, Kwa Kristo.* Naye Kristo inawakilisha vyote tulivyo navyo katika njia ya wokovu na baraka ya kiroho katika Kristo. Katika Kristo inawakilisha umoja wetu pamoja naye, kama shina letu la kila tunachohitaji kumfuata. Maneno haya maneno mawili pia yanawakilisha kujisalimisha kwetu kwa yote yaliyo juu ya moyo Wake, kama wale waliopotea ambao ni lazima wasikize Injili ya wokovu. Kwa kuwa Kristo anawakilisha motisha yetu ya kuishi maisha yetu na Kristo na katika Kristo.

SURA YA KUMI

Uwazi Wa Mhudumu

Waraka wa pili wa Paulo kwa Wakorintho ni kuhusu huduma ambayo Mungu anataka kila muaminifu kuwa na ujuzi wake. Paulo aliwaambia Waefeso kuwa, '*maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo* (**Waefeso 2:10**).' Tumeokolewa kwa neema, bali tumeumbwa kwa ajili ya kazi njema. Au kwa maelezo mengine, Mungu ana huduma kwa ajili yetu na huduma hiyo ni sababu moja kutuleta kwake mwenyewe na katika wokovu. Ingawa kazi hizi haziwezi kutuokoa, ndiyo makusudi katika maisha haya ya wokovu wetu.

Tayari tumejifunza katika somo hili kwamba waumini wote ni wahudumu wa Injili, walioumbwa na Mungu kwa ajili ya kazi nzuri, na kwamba kusudi la huduma yetu ni kuwapatanisha watu wote na Mungu. Lakini ili kuwaleta watu kwa Mungu, maisha yetu ni lazima yawe na tabia ya utu wenye unyofu wa moyo. Ni lazima iwe dhahiri kwa watu wote

kwamba kila kitu chema maishani mwetu ni kwa sababu ya Kristo aliyetuokoa ambaye anaishi ndani yetu.

Je! Mtazamo Wetu Wa Maisha Ni Upi?

Uwazi wa mhudumu unaanzia jinsi anavyotazama maisha yake mwenyewe. Anajitambua mwenyewe kama chombo kinachotumia na Mungu: '*Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. . . siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu (***4:7, 10**).'

Sisi tu vyombo vya udongo, lakini tunabeba hazina kuu yenye thamani ya Yesu Kristo ndani yetu. Kuwa dhahiri kwetu kunaifanya ile hazina kufahamika na watu wengine. Hata zile nyufa kwenye vyombo vya udongo ni sehemu ya udhahiri wetu kuwa hazina yetu ni kama Nuru ambayo hung'aa kutoka katika nyufa zile, au ni ushahidi dhahiri wa unyonge wetu wa kibanadamu.

Ili kutimiza wajibu huu, Bwana huruhusu msukumo kujia vyombo vya udongo. Misukumo hii ni majaribu ambayo tunavumilia kwa ajili ya Injili. Wakati wote Paulo aligusia majaribu yake mwenyewe katika waraka huu ili kuonyesha jinsi yalivyokuwa sehemu ya kumtayarisha kama mhudumu wa Injili. Kristo hujidhihirisha mwenyewe katika majaribu yetu kwa kuwa nguvu zake zinatuwezesha kuvumilia*: 'Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi* (**4:8-9**).' Wakati majaribu yanapotujia nasi kuyakabili, wengine hushangaa ni kipi kinachotuwezesha kuvumilia majaribu hayo. Hivyo basi, tunaweza kushiriki na hazina hii ya thamani kuu ya Kristo.

Seminari (Chuo) Cha Mateso

Paulo aliandika kuwa '*sisi twajithibitisha wenyewe kuwa tu wanafunzi wake Mungu kwa kuyapitia majaribu yetu: Katika dhiki, katika misiba, katika shida, katika mapigo, katika vifungo, katika fitina, katika taabu, katika kufunga* (**6:4-5**).'

Nayataja maovu haya kuwa, ‘dhoruba.’ Ili apate kujidhihirisha mwenyewe, Mungu huwaruhusu wahudumu Wake kukumbana na dhoruba. Huruhusu hata wakati mwingine kuzielekeza kwetu.

Ana aina ya njia ya kipekee ambayo hupendezwa nayo kwa wahudumu Wake ili kukabiliana na dhoruba: ‘*Katika usafi, katika ufahamu, katika subira, katika utu wema* **6).’** (Lakini hii inawezekana vipi?) Kupitia rasilmali ya kiroho ambayo anatupatia: *‘Katika Roho Mtakatifu, katika upendo wa kweli, katika Neno la kweli, katika uweza Wake Mungu; na kwa silaha za haki kwa mkono wa kuume na ule wa kushoto* (**6-7**).’ Kupitia msukumo huu pamoja na kukabiliana kwetu kupitia nguvu za Roho, tunaonyesha Kristo kwa ulimwengu kama wahudumu Wake wa Kweli.

Katika sura ya tano, Paulo anatufungulia dirisha ya motisha yake. Katika sura ya kumi na moja, anatufungulia dirisha lingine la historia ya maisha yake katika Seminari ya kibinafsi ya mateso: *‘Katika taabu kuzidi sana; katika vifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi. Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja. Mara tatu nalipigwa kwa bakora; mara moja nalipigwa kwa mawe; mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini; katika kusafiri mara nyingi; hatari za mito; hatari za mjini; hatari za jangwani; hatari za baharini; hatari za ndugu wa uongo; katika taabu na masumbufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi* (**11:23b-27**).’ Kupitia majaribu haya na makabiliano yake kwao, Paulo aliweza kujithibitisha kama mhudumu wa Injili.

Je! Watu wanafahamu vipi ikiwa wewe ni mhudumu wa Mungu? Watu hutamani kuona jinsi maisha ndani ya Kristo yalivyo tofauti na bila Kristo? Je! Wanaona Hazina anayeishi ndani ya chombo chako cha udongo? Huduma ya Injili si kuhusu kile Paulo anachotaja kama, *‘Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu* (**4:2**).’ Huduma ya kweli ni kuhusu ushuhuda dhahiri wa maisha yetu – kwamba tunateseka kwa ajili ya Kristo lakini tunaweza kustahimili mateso hayo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Maisha ya wahudumu yanastahili kuwa ushuhuda wa Kristo kwa wale wanaomtazamia kama Mwokozi.

SURA YA KUMI NA MOJA

Kukuzwa Kwa Mhudumu

Ushuhuda Kwenye Njia Ya Dameski

Ni vigumu kuelewa maisha ya Mtume Paulo pasipo kuambatana na neno, 'ushuhuda.' Paulo alikuwa na ushuhuda kadhaa katika maisha yake humu ulimwenguni. Kabla ya kugeuzwa katika Ukristo, alitesa Kanisa kwa juhudi kuu. Kwa 'maono ya tundu' – yaliyoelekezwa kwa jambo moja tu, vile Sauli wa Tarso alivyojitolea katika uharibifu wa kizazi cha kwanza cha Kanisa la Yesu Kristo. Lakini baadaye alipokea ushuhuda wa Kristo akiwa njiani kuelekea Dameski, ambapo alizungumza moja kwa moja na Kristo,na kumpofusha macho yake kwa mwangaza mkuu (**Matendo 9**). Ushuhuda wa njiani kuelekea Dameski ulibadilisha maisha ya Paulo wa Tarso milele!

Ushuhuda Katika Jangwa la Arabuni

Kabla ya Paulo kuanza huduma yake kwa watu, alikwenda huko jangwani la Arabuni, na kupata ushuhuda mwingine. Huko Arabuni, alijifunza mambo yale aliyostahili kujifunza kwa ajili ya huduma, huku akichagua kutoshauriana na watu kama mitume, bali na Kristo aliyefufuka, Mwenyewe (**Wagalatia 1,2**). Wasomi hawakubaliani kuhusu muda aliokuwa pamoja na Kristo huko jangwani. Baadhi yao husema miaka mitatu ilhali wengine wanaamini kwamba inawezekana kuwa ilikuwa ni kwa muda mrefu zaidi. Mitume waliishi kwa miaka mitatu na Yesu akiwa kama mwalimu wao, ilhali Paulo pia alidai kwamba aliishi kwa miaka sawa na hiyo na Yesu huko jangwani la Arabuni. Ushuhuda huu wake katika jangwa la Arabuni ulimtayarisha kuandika nusu ya Agano Jipya na kuieneza injili kote ulimwenguni siku zake.

Ushuhuda Wa Mbinguni

Paulo alinakili ushuhuda wake wa tatu katika **2 Wakorintho 12,** pale alipotuambia kuwa alinyakuliwa juu kwenda mbinguni ya tatu. Hakutoa maelezo mengi kuhusu ushuhuda huu, ila alisema kuwa, *'Aliyasikia mambo yasiyokubaliwa kunenwa, na ambayo mwanadamu haruhusiwi kuyanena* (**4**).' Paulo alishiriki ushuhuda huu wa mbinguni pamoja na Wakorintho ili kuonyesha cheti chake kama mhudumu wa Injili. Ushuhuda huu ulimshawishi kwamba inawezekana kuishi katika hali ya mbinguni hali tunaishi humu

ulimwenguni. Kuishi na kuenenda kwa mhudumu na kuwa na utu wake katika hali ya mbinguni ni kile tunachomaanisha kama ‘kukuzwa kwa mhudumu.’

Mtazamo Wa Mbinguni

Ushuhuda wa Paulo katika mbingu ya tatu ulimwacha alama ya kudumu katika maisha yake. Tangu wakati huo, alikuwa kana kwamba alikuwa na mguu mmoja huko mbinguni ilhali ule mwingine hapa duniani. Alizungumzia wakati mwingi kuhusu hamu yake kutoka duniani na kuwa na Kristo, huku akihesabu maisha yake humu ulimwenguni kama kuwa hayana thamani kuliko utukufu wa kuwa na Kristo huko mbinguni **(Wafilipi 1:21-24**).

Ushuhuda huu uligusia mtazamo wa maisha ambao aliushiriki na watu wengine. Wakati alipoandika Waefeso, ni dhahiri kwamba yeye aliwataka wao kuiweka mbingu mbele ya mawazo yao huku akiandika hivi: ‘*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo* (**Waefeso 1:3**).’ Aliwaandikia Wakorintho kwamba ikiwa katika maisha haya tunalo tumaini kwa Kristo tu, basi twahitajika kuhurumiwa kati ya wanadamu wote (**1 Wakorintho 15:19**).

Mtazamo Wa Unyenyekevu

Katika sura ya kumi na mbili ya waraka huu, Paulo anatufungulia dirisha lingine katika historia ya maisha yake. Aliwaambia Wakorintho kwamba alipewa ‘mwiba mwilini mwake’ ambao ulikuwa ni ‘*mjumbe kutoka kwa shetani ili kumuumiza na kumsumbua, na kukitoboa kiburi chake* (**7**).’ Wasomi hawakubaliani kuhusu mwiba huu uliokuwa nini. Tunafahamu kuwa alikuwa amewaandikia Wagalatia, kuwa macho yake hayakuwa mazuri kutokana na tukio lisilopendeza hivi kwamba kama ingewezekana wangelimpa macho yao (**Wagalatia 4:15**).

Katika nyaraka zake kwa Wakorintho, alizungumzia kuhusu uchovu ulioambatana na wakati wote. Aliwaambia kwamba alifikiria kuwa kuwepo kwake katika mwili kulikuwa na unyonge huku akiwakumbusha kwamba alikuwa pamoja nao katika unyonge huo (**2 Wakorintho 10:10; 1 Wakorintho 2:3**). Kwa kuwa aliandika nusu ya Agano Jipya, na

kuanzisha Makanisa kote ulimwenguni. Huku akiwa na ujuzi mwingi usio wa kawaida pamoja na Kristo aliyefufuka, alituambia kuwa Mungu alimdhania kuwa mwenye kiburi. Kulingana na Paulo, Mungu aliruhusu ‘mwiba wake mwilini’ ili kumfanya mnyenyekevu.

Je! Mungu amekupa mwiba mwilini mwako? Je! Unakumbana na vizuizi ambavyo hukufanya kuhisi kwamba Mungu hawezi kukutumia? Upokee ujuzi wa Paulo ili upate kuhimizwa. Mungu hupenda kutumia unyonge au udhaifu wetu kama ishara ya maonyesho ambapo anaweza kudhihirisha uwezo Wake. Mungu hupenda kuonyesha kutopungukiwa kwake kwa kukuonyesha kupungukiwa kwetu. Mungu atatumia upungufu kwako ili kukuonyesha pamoja na wengine kwamba sio hoja kuwa wewe ni nani, au kile tulicho nacho bali Yeye ni nani. Kumtumikia Mungu hakuhusu kile tuwezacho kutenda au kile hatuwezi kutenda. Mshukuru Mungu kwa kuwa amekupa nguvu ingawa wewe ni mnyonge. Mruhusu kudhihirisha uwezo Wake katika maisha yako, jinsi haujaikuwa na ujuzi hapo awali.

SURA YA KUMI NA MBILI

Neema Ya Matoleo

Kuna funzo moja la Paulo katika waraka huu wa pili kwa Wakorintho ambalo twahitajika kutilia mkazo tunapomalizia ukaguzi wetu wa waraka huu. Kabla ya Paulo kubadilika na kuwa Mkristo, alikuwa Mfarisayo mwenye juhudi kuu ambaye alikuwa amejitolea kutunza na kuilinda dini na imani ya Kiyahudi. Kwa kuwa alikuwa amemkataa Kristo na kuwadhulumu wafuasi Wake kama kuwa ni tisho kwa imani ya Kiyahudi, aliwatesa sana Wayahudi waliokuwa wanafunzi wa Yesu Kristo. Baada ya kuokolewa na Kristo, huenda alikuwa mwenye hukumu na msumbufu kwa ajili ya vifo na mateso mengi aliyowaelekeza waumini kama Stefano. Wanafunzi wa Kiyahudi wa Yesu huko Yerusalemu na Uyahudi walikuwa katika dhiki na janga kuu la njaa. Jinsi tulivyojifunza katika sura ya mwisho ya waraka wa kwanza kwa Wakorintho, Paulo alijawa na huruma kwa ajili ya hawa waumini wa Kiyahudi kiasi kuwa aliwaagizia matoleo ya upendo kutoka kwenye Makanisa ya Mataifa. Kweli kwamba huyu mtesi wa zamani wa Wayahudi ambaye alikuwa akimfuata Yesu Kristo wakati huu alikuwa akipokea matoleo ili kuwasaidia waliokuwa wakiteseka, ni ushuhuda wa muujiza wa neema ya Mungu katika kubadilisha maisha.

Paulo aliandika kwa Wakorintho kuhusu matoleo haya ya upendo katika (**2 Wakorintho 8-9**), huku akiwauliza kutoa matoleo yao kwa upendo wao kwa ndugu waliokuwa wakipitia dhiki. Alishiriki nao kuhusu tabia ya Wafilipi ya matoleo, ambapo alikuwa akiishi katika mji wao wakati alipokuwa akiwaandikia waraka huu, kwani wao walikuwa mfano bora katika matoleo yao na wakili waaminifu. Safari za Paulo za kimishionari zilisimamiwa na msaada wa waumini wa Filipi, ambao walikuwa wamekomaa kabisa katika imani yao hivi kwamba alipata kufahamu kuwa motisha ya matoleo yao ilikuwa nzuri na kuwa walikuwa na ufahamu bora kuhusu maana ya uwakili uaminifu. Wafilipi pia walikuwa wamefanya matoleo yao ya fedha kwa watakatifu waliokuwa wakiteseka huko Yerusalemu, ambayo Paulo aliyanakili katika waraka huu wa Wakorintho:

'Tena ndugu zangu, twawaarifu habari ya neema ya Mungu, waliyopewa makanisa ya Makedonia; maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao. Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao; wakituomba sana pamoja na shirika hili la kuwahudumia watakatifu. Tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu. Hata tukamwona Tito kuwatimilizia neema hii kwenu kama vile yeye alivyotangulia kuianzisha.

Lakini kama mlivyo na wingi wa mambo yote; imani, na usemi, na elimu, na bidii yote, na upendo wenu kwetu sisi; basi vivyo hivyo mpate wingi wa neema hii pia (**8:1-7**).'

Paulo ainua utumishi wa Wafilipi kama ndio mfano kwa Wakorintho. Alipenda sana Kanisa hili la Filipi ilhali Kanisa la Korintho lilikuwa ndilo lililokuwa na utata sana. Huku Paulo akielezea uaminifu wa Wafilipi kwa Wakorintho, anatupatia somo kuu kuhusu uwakili wenye uaminifu. Hapa kuna ufupisho kuhusu mfumo wa uwakili wa Kanisa la Filipi, ambalo Paulo alikuwa ameuhimiza wakati alipoufanya kuwa sehemu ya pili ya waraka wa pili kwa Wakorintho.

Thamani Ya Uwakili Wenye Uaminifu

Paulo alisema kuwa Wafilipi *‘kwanza walijitolea kwake Bwana na baadaye wakajitolea kwetu kulingana na mapenzi yake Mungu (**5**).’* Paulo hangekubali matoleo kutoka kwa watu bila kuambatana na masharti haya. Wao walihitajika kujitolea kwa Mungu kwanza kabla ya kutoa sehemu yao kwa mwanadamu. Wafilipi walikuwa wamejitolea kwa Paulo tu baada ya Mungu kuthibitisha kuwa ilikuwa ni kuambatana na mapenzi Yake kutenda hivyo.

Hata hivyo, Wafilipi waliyafanya matoleo yao kwa hiari yao wenyewe, huku wakimsihi kuwa na fursa ya kushiriki katika huduma hii kwa Wayahudi waliokuwa wafuasi wa Kristo, ambao walikuwa wakiteseka. Huu ni mtazamo mwingine muhimu kuhusu thamani ya mchango wetu. Paulo hangemlazimisha wala kumhadaa mtu ye yote kushiriki katika mchango huu kwa kuwa aliwataka wao kuchanga kwa hiari yao wenyewe. Jinsi anavyoandika katika sura inayofuata: *‘Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu* (**9:7**).’

Uwezo Unaohusika Katika Uwakili Wenye Uaminifu

Paulo alisema kuwa Wafilipi walifanya mchango wao kwa ukarimu, *‘Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao* (**8:3**).’ Tunafahamu kuwa walikuwa hawana mali nyingi kwa kuwa Paulo alikuwa amesema kwamba wao walikuwa katika ‘umasikini mkuu (**2**).’ Wakati mtu anapofanya mchango wake kwa ukarimu, mara nyingi sisi hudhania kwamba ni tajiri. Yaonekana kwamba itakuwa rahisi sana kwake tajiri kufanya matoleo yake kutokana na wingi wa mali yake. Lakini hivyo sivyo ilivyo kwa hawa Wafilipi. Wao waliyafanya matoleo yao katika wakati wa umaskini mkuu na majaribu mengi – na walikuwa wakiyatoa zaidi ya uwezo wao.

Yawezekana vipi kwa muumini kutoa matoleo kupita uwezo wake? Ni kwa kuruhusu neema ya Mungu kufanyika zaidi katika vipawa vyao. Tunapofanya uamuzi wa kile tunachofahamu kwamba tunaweza kutoa kwa kazi ya Bwana, lakini tunamwuliza kutuongezea neema Yake kwa kipawa hicho, basi tunaweza kumwona Mungu akitenda kazi

Yake kupitia imani yetu. Kwa neema Yake, anaweza kutuongezea kile tunachomtolea katika imani.

Wafilipi katika umaskini wao, walitoa vipawa vyao vidogo kwa Mungu na kushuhudia vikikua huku neema Yake ikivifanya kuwa zaidi ya uwezo wao wa kutoa. Hili ndilo Paulo alilomaanisha wakati aliposema, *'Tena ndugu zetu, twaarifu habari ya neema ya Mungu, waliyopewa makanisa ya Makedonia* (**1**).' Neno linalotumika hapa kwa neema ni *'charis,'* au *'charisma,'* ambalo linamaanisha nguvu na baraka za Mungu juu ya maisha ya mtu. Ni neema ya Mungu ambayo hutufanya kuchanga zaidi ya uwezo wetu wa kibinadamu. Hii ndio maana ya neema ya kutoa.

Usawa Wa Uwakili Uaminifu

Wakati Paulo alipowakaribisha Wakorintho kushiriki katika mchango wake wa upendo kwa waumini waliokuwa wakiteseka huko Yerusalemu na Uyahudi, aliandika: *'Maana sisemi hayo, ili wengine wapate raha nanyi mpate dhiki; bali mambo yawe sawasawa wakati huu wa sasa wingi wenu uwafae upungufu wao, ili na wingi wao uwafae ninyi mtakapopungukiwa; ili mambo yawe sawa. Kama ilivyoandikwa, Aliyekusanya vingi, hakuzidi, wala yeye aliyekusanya vichache hakupungukiwa* (**8:13-15**).'

Mchango unahitajika kuambatana na mapato ya mwenye kutoa, wala sio yale waumini wasio nayo. Mungu anaweza kufanya kipawa kulingana na kipimo cha dhabihu iliyofanywa katika mchango huo. Tunapofanya mchango kulingana na kile tulicho nacho kwa imani, ingawa ni vigumu na hatuna kingi cha kutoa, Mungu anaweza kufanya mara dufu kwa njia nyingi hili iwe thamani ya kipawa kikubwa ambacho kimetolewa na tajiri kwa wepesi mno. Matunda ya kipawa hayategemei kiwango kilicho tolewa, bali katika imani na kujitolea kabisa kulikotumika kukitoa.

Hili ndilo funzo ambalo lililotolewa na Yesu wakati aliposema kwamba yule mjane maskini aliyekuwa amekitoa kipawa kidogo kwa hakika, ndiye amechanga sana kuliko wote waliokuwa wamechanga nyingi kwa kuwa alitoa chote kilichokuwa tegemeo la uhai wake (**Luka 21:1-4**).

Je! Na wewe je? Je! Unatambua kwamba kile ulicho nacho ni mali ya Mungu na kuwa Anakuuliza kuwa wakili mwema kwa vitu hivyo? Je! Unafanya mchango wako kwa uchangamfu kwa kazi ya Bwana? Je! Unatoa mchango wako kwa kujitolea mhanga? Uwe mwaminifu na kile ulicho nacho, naye Mungu atakitumia kubariki ufalme Wake – hilo ndilo ahadi Lake.